SportPesa
TZS. 450,150,500
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Gwajima** agoma kukaa, ahojiwa akiwa amesimama

UKURASA 3


ama
ALHAMISI AGOSTI 26, 2021
AFYA NA MAZINGIRA
Baada ya GBV, kuwaathiri kiafya, kinamama waungana kuikabili
Wajawazito mmesikia ni ruksa kuchanjwa UVIKO- 19 ila...
Kuupuuza UVIKO-19 sasa kwaiibua CHAKUA
•Wajitosa ndani ya vyombo vya usafiri, stendi

UKURASA 11

Nipashe
Alhamisi Agosti 26, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580684
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# UTATA MAUAJI DAR

UKURASA 2



Mwili wa mtu asiyejulikana aliyekuwa na silaha aina ya bunduki na kupiga risasi ovyo na kusababisha vifo vya watu wanne, katika eneo la jirani na Ubalozi wa Ufaransa, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, mkoani Dar es Salaam jana, ukiwa umelala chini baada ya kufariki dunia wakati wa majibizano ya risasi na polisi. Picha ndogo: Askari polisi wakiimarisha ulinzi eneo la tukio. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Rais Samia awashukia polisi vifo watuhumiwa



UKURASA 3

## ICU JKCI yazidiwa wagonjwa

• **Prof.** Janabi asema hajawahi kushuhudia vifo vingi kama ilivyo sasa...*Endelea ukurasa 2*

**MICHEZO** **YANGA YAFUNGUKA KAZI ZA MANARA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# ICU JKCI yazidiwa

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Prof. Mohammed Janab, amesema janga la corona limesababisha vyumba vyao vya Uangalizi Maalum (ICU) kujaa wagonjwa na kushauri wananchi wachanje badala ya kusubiri wafikishwe hospitali wakiwa na magonjwa zaidi ya moja.

Prof. Janab alitoa ushauri huo juzi jioni wakati akitoa elimu ya chanjo na athari zitokanazo na corona kwa wafanyakazi wa shule binafsi ya International School of Tanganyika (IST) iliyoko Upanga jijini Dar es Salaam na baada ya mafunzo hayo, utolewaji wa chanjo kwa hiari ulifanyika shuleni huko.

Akijibu swali la mmoja wa wafanyakazi wa shule hiyo aliyetaka kujua muda wa kutumia dawa kwa mtu mwenye shinikizo la damu endapo akiamua kuchanjwa, Prof. Janab alisema mtu huyo anaweza kuchanja na kuendelea na dozi yake.

Prof. Janab alifafanua kuwa mtu mwenye tatizo la shinikizo la damu, atapata kiharusi ikiwa ataacha kutumia dawa.

"Dawa za shinikizo la damu haziachwi hata dakika moja, shinikizo la damu linaharibu mishipa ya damu, corona inaharibu mishipa ya damu, ninatamani upate muda hata kesho (jana) upite JKCI nikuonyeshe namna ICU zilivyojaa.

"Uje uone watu wanavyoteseka ICU zetu zote hazina nafasi kwa sababu kuna wagonjwa wa COVID-19, ninakupa elimu leo, uamuzi wa mwisho ni wako kuchanja au kutochanja," alisema.

Prof. Janab aliwataka wafanyakazi hao wajiulize wapate corona huku tayari wana maradhi mengine mwilini yanayowasumbua au wajikinge na janga hilo.

"Kipi kirahisi upate corona na shinikizo la damu? Au uje ukiwa na ugonjwa wako wa shinikizo la damu au mwingine tukutibie?

"Nilikuwapo wimbi la kwanza, wimbi la pili, wimbi la tatu sitaki kukumbushia watu waliopoteza maisha, sio kupinga, ni maisha ya watu yanapotea, hatujawahi kupata vifo vingi namna hii, ni uamuzi wa kila mmoja wetu," alisema.

Aliwaondoa hofu wale wanaohofia chanjo kwa kuwaeleza kuwa chanjo zilizopitishwa ni salama.

"Kama mnaniamini mimi, mnaniletea ndugu zenu au ninyi wenyewe, ninafanya upasuaji mkubwa wa moyo, tunausimamisha kwa saa nne au sita halafu ninaupiga umeme uanze tena kufanya kazi, ninaomba mtuamini kwenye hili la chanjo tunachowaeleza," Prof. Janab alisema.

Pia alisema matatizo yaliyopo duniani kwa sasa mahitaji ya chanjo ni makubwa kuliko uzalishaji ndiyo maana nchi zilizoendelea wamelipia huduma hiyo hadi mwakani.

Prof. Janab alitaja takwimu za watu waliojitokeza kuchanjwa katika kituo cha kutolea chanjo kilichoko JKCI na kueleza kuwa hadi siku hiyo, walikuwa zaidi ya 3,500 na kwamba hakuna aliyerudi na kusema amepata matatizo baada ya huduma hiyo.

"Kwa miaka karibu miwili tulichojifunza hautakiwi (corona) ikukute na kitu chochote, haitaki watu wazima, wengi waliofariki ni hao wenye matatizo mengine, ndiyo maana kwa yule mwenye kisukari, shinikizo la damu, figo, saratani, chanjo zilivyokuja tulisema wawe mstari wa mbele kwa sababu ukikukuta na chochote katika hivyo kwa lugha ya mtaani (virusi) vinapata kichaa," alisema.

Mkurugenzi wa IST, Mark Hardeman, alisema shule hiyo imeamua kumwita mtaalamu huyo kutoa elimu ya corona na chanjo kwa wafanyakazi wake baada ya kuridhika na juhudi za Serikali ya Tanzania katika kupambana na janga hilo kwa kuhamamsisha wananchi wakachanje.

"Tumeamua kuwa sehemu ya mapambano hayo kwa kuwawezesha wafanyakazi wetu kupata mafunzo dhidi ya corona na chanjo zinazotolewa ili na wao waamue kuchanja kwa hiari yao," alisema.

Hardeman alisema wana wafanyakazi takribani 260 ambao anaamini elimu iliyotolewa kwao itawawezesha kutambua umuhimu wa kujilinda wao wenyewe na jamii kwa ujumla.

Nipashe ilishuhudia baada elimu hiyo idadi kubwa ya wafanyakazi walioitikia wito wa serikali kuchanja kwa hiari shuleni huko.

# Utata mauaji askari Dar

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameliagiza Jeshi la Polisi kuchunguza tukio lililojaa utata la mauaji ya askari wanne walioshambuliwa na kijana mwenye silaha eneo la Selander jijini Dar es Salaam jana.

Katika tukio hilo ambalo watu wengine sita wamejeruhiwa, kijana mwenye silaha ambaye baada ya kufanya mauaji hayo aliuawa na Jeshi la Polisi, anadaiwa kufika eneo hilo na kuanza kufyatua risasi ovyo na kusababisha taharuki kwa watumiaji wa barabara hiyo.

Kutokana na tukio hilo, Rais Samia ametoa pole kwa Jeshi la Polisi na familia za askari polisi watatu na askari mmoja wa Kampuni ya Ulinzi ya SGA waliopoteza maisha baada ya mtu huyo mwenye silaha kuwashambulia.

Kupitia ukurasa wake rasmi wa Twitter jana, Rais ameliagiza Jeshi la Polisi kuchunguza kwa kina tukio hilo huku akieleza kuwa mtu huyo amedhibitiwa na hali ni shwari.

Awali, Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, alisema mtu huyo aliwaua askari wawili.

"Aliwapiga risasi wote wawili, akaingia barabara kuu akawa anatamba na SMG naye akapigwa risasi na askari wetu, askari wetu wamefariki na yeye huyu bwana amefariki.

"Tunaendelea kufuatilia kujua namna gani, lakini challenge (changamoto) tuliyonayo ni kwamba kama mnavyojua kule Msumbiji kuna shida.

"Majeshi yetu yapo kule, ni suala la kujipanga, tumepoteza askari wetu wawili lakini huyu Bwana aliyefanya mauaji hayo tunataka kujua ametoka wapi, ni nani? Baadaye nitawapa taarifa," aliahidi.

Kamishna wa Operesheni na Mafunzo ya Jeshi la Polisi, Liberatus Sabas, alisema wakati askari wakiwa kazini, alifika mtu huyo akawashambulia kwa silaha aina ya bastola kisha akachukua silaha mbili akaanza kurusha risasi ovyo kuelekea Ubalozi wa Ufaransa.

Alisema alipofika ubalozini kuna kibanda akajibanza na kuanza kufyatua risasi ovyo na kuua askari wanne na kujeruhi watu sita ambao wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

"Uchunguzi utabaini (sababu), tumeshaanzisha timu ya upelelezi na muda sio mrefu tutakamilisha," alisema.

**WALIOSHUHUDIA**

Askari anayefanya kazi Ubalozi wa Ufaransa, ambaye hakupenda jina lake liandikwe gazetini, alisimulia kuwa wakati tukio linatokea ilikuwa majira ya saa 5:30 asubuhi ambapo walianza kusikia milio ya risasi ikitokea nje ya geti lao.

"Sisi tulikuwa ndani, milio ya risasi ilianza kusikika maeneo ya Selander, wakati huo tulikuwa askari wawili wa kampuni na nje walikuwa askari polisi ambao wakati huo walikwenda kudumisha nguvu maeneo ya Daraja la Selander ambao pia wanakujaga hapa maeneo ya ubalozi. "Wakawa wameondoka, wamekwenda kule baadaye ndiyo tukasikia hizo sauti za milio ya bunduki wakati hao askari hawapo, tulipochungulia tukaona kuna mashambulio yanaendelea, tukatoa taarifa kwa bosi wetu," alidai.

Alisema baadaye aliona mtu huyo akikimbilia maeneo ya kibanda cha askari polisi nje ya jengo hilo ndipo baadhi ya askari polisi wakamshambulia wakiwa wanatupiana risasi.

"Mpaka anauawa yalikuwa ni mashambulizi kati ya askari polisi na huyo mtu ambaye mpaka sasa hatujui alikuwa na shida gani," alisema.

Shuhuda mwingine, Maziku Mohamed alidai kijana aliyefanya mauaji hayo alitokea eneo la Daraja la Selander, akaingia kwenye kibanda cha askari, akachukua silaha ya askari polisi na kuwajeruhi kisha kwenda eneo la Ubalozi wa Ufaransa.

Alidai mtu huyo alianza kurusha risasi akijibizana na askari polisi na kusababisha taharuki eneo hilo, magari yakishindwa kupita.

"Alikuwa peke yake, ana asili kama ya Kisomali hivi lakini polisi walimzunguka, kwa hiyo kama unavyoona yupo chini," alisema.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) jana kilitoa salamu za rambirambi kwa IGP Sirro na familia zilizopoteza ndugu zao kutokana na tukio hilo.

"Tunaomba Watanzania wawaombee majeruhi wote ili waweze kupona na kuendelea na majukumu ya kujenga taifa," ilisomeka sehemu ya taarifa ya chama hicho iliyotolewa na Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje, John Mrema.



Mwili wa kijana aliyeuawa baada ya kuua askari wanne ukiwa eneo la tukio. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## HABARI KITAIFA

# Samia awashukia polisi vifo watuhumiwa vituoni

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amelitaka Jeshi la Polisi kukaa na wadau kuangalia uwezekano wa kurekebisha sheria ya kuweka mtu mahabusu.

Amesema kucheleweshwa kwa upelelezi kunaongeza mzigo mkubwa kwa serikali kuweka mahabusu jela.

"Tukiangalia takwimu hadi mwezi huu tarehe 22, idadi ya mahabusu katika jela zetu ni karibu na idadi ya wafungwa katika jela zetu.

"Wafungwa walikuwa 16,542 lakini mahabusu 15,194 mpaka juzi, sasa mahabusu hawa wapo waliokaa wiki, miaka miwili, miaka mitatu, mwaka na muda mbalimbali," Rais Samia alisema jana Dar es Salaam wakati akifungua kikao kazi cha maofisa wa polisi.

Alitoa wito kwa jeshi hilo kwa zile kesi ambazo wanaona upelelezi wake hautokamilika, watuhumiwa hao watolewe jela wakafaidi uhuru wao wakiwa nje.

"Kama kesi haina mwelekeo, na hili ninalisema kwa mara ya pili ama mara ya tatu, basi hao watu watolewe, lakini kwa zile kesi ambazo una uhakika upelelezi utatimia, basi mharakishe kama mlivyojiwekea muda miezi sita mpaka mwaka.

"Lakini kwa upande mwingine mwanadamu ni mwanadamu na ana uhuru wake, ninaomba mkae na wadau wengine mwangalie uwezekano wa kurekebisha sheria ya kuweka mtu mahabusu.

"Kwenye nchi nyingine mtu hakamatwi mpaka upelelezi umetimia, akikamatwa anawekwa ndani wiki, siku tatu nne tayari mahakamani anahukumiwa anaendelea," alisema.

Rais alibainisha kuwa baadhi ya askari polisi wanatuhumiwa kutotenda haki kwa jamii, akitolea mfano tukio la baadhi yao kudaiwa kunyang'anya nyama kutoka kwa wafanyabiashara wa nyama jijini Dar es Salaam na kugawana.

### WATUHUMIWA KUFA KITUONI

Rais Samia pia alizungumzia suala la watuhumiwa kufia mikononi mwa polisi, akisema: "Mtuhumiwa anapokufa mikononi mwako askari wa polisi, umemchukua huko, umemburuza, umemchapa virungu, wanadamu sisi tupo wa afya tofauti tofauti. Kuna mwingine utamchapa lakini yupo ngangari, mwingine vifimbo viwili tu ashafika mbele za haki.

"Kwa hiyo nadhani matumizi makubwa ya nguvu, IGP (Mkuu wa Jeshi la Polisi) na lenyewe mlitazame. Kesi za kufa watu vituo vya polisi hazileti picha nzuri, ninaomba sana ndugu zangu tendeni yalio haki."

Rais pia aliliagia jeshi hilo kuwafikia wananchi na kushughulikia matatizo yao ipasavyo ili kuzuia wananchi kujichukulia sheria mkononi.



Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima akihojiwa na Wajumbe wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, huku akiwa amesimama baada ya kugoma kukalia kiti alichoandaliwa jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Gwajima ahojiwa akiwa amesimama

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, imekamilisha kumhoji Mbunge wa Kawe (CCM), Askofu Josephat Gwajima, safari hii akihojiwa akiwa amesimama.

Imesema tayari imeshapata taarifa ilizokuwa inazitaka kutoka kwa shahidi huyo.

Kamati hiyo pia imeanza kazi ya kuchambua na kufanya majumuisho ya hoja ilizoziona na haitazuia kumwita tena shahidi huyo kama kutakuwa na jambo la ziada linalohitaji ufafanuzi.

Akizungumza baada ya kumhoji mbunge huyo jana, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Emmanuel Mwakasaka, alisema kwa sasa kamati imekamilisha kumhoji shahidi huyo na baada ya kamati kumaliza kazi yake, itawasilisha taarifa kwa Spika wa Bunge, Job Ndugai, ambaye ndiye aliyepeleka shauri kwa kamati.

"Tumemsikiliza Askofu Gwajima, shauri lake limeisha, kazi inayoendelea ni majumuisho ya tulichokiona lakini haizuii kama kuna jambo la ziada ataitwa, kwa sasa kazi imeisha," alisema.

Askofu Gwajima alihojiwa jana kwa mara ya pili ikiwa ni mwendelezo wa mahojiano yaliyofanyika Agosti 23, mwaka huu.

### AHOJIWA AKIWA AMESIMAMA

Mbunge huyo aliingia ukumbini saa 8:29 mchana na kusogeza kwa mguu kiti kilichokuwa kimeandaliwa kwa ajili yake na kutaka ahojiwe akiwa amesimama kwa madai ya kuwa angekuwa huru zaidi.

"Samahani Mwenyekiti, kwa leo nitasimama na nimeamua kwa sababu nimezoea na nipo 'comfortable' kuongea nikiwa nimesimama kama itakupendeza," alisema.

Kufuatia ombi hilo, Mwakasaka alikubali hoja yake na kumhoji sababu ya yeye kusimama badala ya kukaa.

"Shahidi tunaomba utueleze sababu ya kusimama kama una ugonjwa wowote unakusumbua au tatizo lolote lakini kama upo huru, sawa unaweza kusimama," alisema.

Kabla ya kuhojiwa, Gwajima aliulizwa na waandishi wa habari sababu za kugoma kukalia kiti kilichoandaliwa, akisisitiza hawezi kusema chochote kuhusu hilo.

Agosti 21 mwaka huu, Spika Ndugai aliamuru Askofu Gwajima na Mbunge wa Ukonga, Jerry Silaa, kuhojiwa na kamati hiyo ili kujibu tuhuma mbalimbali ikiwamo uongo na kushusha hadhi na heshima ya Bunge.

Wabunge hao walitakiwa kufika mbele ya kamati kwa mujibu wa kanuni ya 4(1)(a) na (b) ya nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Juni 2020 ambayo inaipa mamlaka kamati hiyo kuchunguza mambo yanayohusu maadili ya wabunge yanayopelekwa kwa Spika.

Leo kamati hiyo inatarajiwa kuendelea na mahojiano kwa mara ya pili na Mbunge Silaa kuanzia saa tano asubuhi.

# Bil. 173/- zatumika kulipa watumishi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema kuanzia Mei, mwaka huu hadi sasa, serikali imetumia Sh. bilioni 172.614 kulipa madeni mbalimbali ya watumishi wa umma.

Pia amesema serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hilo ili lisiendelee kuwa kero kwa wastaafu katika kumudu maisha baada ya kukoma utumishi wao.

Majaliwa alisema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) uliofanyika katika ukumbi wa Hoteli ya Royal Village, jijini Dodoma.

Waziri Mkuu pia aliuagiza uongozi wa TALGWU kutumia fedha na rasilimali za chama hicho kwa kuwahudumia wanachama wao wote bila ubadhirifu.

"Ninawaagiza waajiri wote wazingatie Kanuni za Kudumu Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 ili kuondoa changamoto ya watumishi kutolipwa gharama za kurejeshwa nyumbani na stahili zao zingine baada ya kustaafu," alisema.

Alitoa wito wanaTALGWU na kuwasihi waendelee kushirikiana, kushikamana na kuwajibika kwa kuzingatia uadilifu kwa kuwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi ni silaha kuu katika kufikia malengo ili kupunguza mzigo kwa serikali. Kadhalika, aliwataka viongozi watakaoibuka kidedea katika uchaguzi waliotarajia kuufanya jana, wahakikishe wanakwenda kutekeleza majukumu yao ya kikatiba kwa weledi na kwa kuweka mbele maslahi ya wanachama.

"Natambua kuwa harakati za uchaguzi zinapitia mchakato mkubwa wenye mambo mengi. Hata hivyo, nawasihi baada ya uchaguzi huu mkaimarishe umoja na mshikamano kwani hizo ndizo silaha kuu za kutetea haki na kuimarisha maslahi ya wafanyakazi nchini," alisisitiza.

Kuhusu ugonjwa wa corona, Waziri Mkuu aliwataka wananchi wafuate maelekezo yanayotolewa na wataalamu wa afya katika kujikinga na ugonjwa huo na pale wanapoona dalili ambazo hawazielewi, wawahi katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa uchunguzi na matibabu. Alisema kuwa chanjo ya corona inapatikana na inasambazwa nchini kote ikiwamo Dodoma ambako inatolewa katika vituo 89 ndani ya mkoa.

"Niwatoe hofu wananchi wote kuwa chanjo hii ni salama, haina madhara yoyote na ni hiari wala hakuna atakayechanjwa pasipo ridhaa yake. Niwaombe wananchi kujiepusha na watu wanaopotosha ukweli kuhusu suala la chanjo," alisisitiza.

Naye Katibu Mkuu wa TALGWU, Rashidi Mtima, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuchukua hatua madhubuti kwa lengo la kuondoa kero na kuimarisha maslahi ya wafanyakazi nchini.


**High Commission for Pakistan, Dar es Salaam, United Republic of Tanzania**

**Invitation to attend the "Pakistani Contemporary Art" exhibition at the National Museum of Tanzania on August 28-29, 2021 to commemorate the 75th Independence Day of Pakistan 2021 (August 14)**

To commemorate the 75th Independence Day of Pakistan an special "Pakistani Contemporary Art" exhibition comprising painting and calligraphy works of 35 Pakistani renowned artists is being held in the National Museum of Tanzania in Dar es Salaam from 1000-1500 hours on August 28-29, 2021.

The exhibition would be open for art lovers, media persons and culture fans from 1000-1500 hours on **August 28-29, 2021.**

**Dar es Salaam**
**August 25, 2021**

116425102

# Mhitimu ualimu adaiwa kujinyonga, aacha ujumbe

**Na Thobias Mwanakatwe**

MHITIMU wa ualimu ngazi ya astashahada, Ezekiel Kitumbo (26), anadaiwa kujiua kwa kujinyonga na kuacha ujumbe akiwasihi wazazi wake kuzingatia matumizi ya barakoa.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Rashid Ngonyani, Kitumbo ambaye ni mkazi wa Mtaa wa Majengo, Kata ya Ichenjezya, Mbozi mkoani Songwe, mwili wake uligundulika juzi asubuhi saa 1:00 asubuhi ukining'inja juu ya mti.

Alisema mtu huyo alitumia waya wa kusukia umeme kujinyonga katika mti ulioko karibu na nyumbani kwao katika mtaa wa Majengo.

Kamanda Ngonyani alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa Kitumbo alikuwa na homa kali japokuwa hakwenda hospitalini kupima na kupata matibabu.

"Baada ya kuupekua mwili wa marehemu, mfukoni tuliukuta ujumbe mfukoni uliowasihi wazazi wake kuzingatia matumizi ya barakoa. Baada ya mwili kufanyiwa uchunguzi, ulionyesha alikuwa na homa kali japo haijabainika ni ugonjwa gani," alisema.

Aliongeza kuwa mwili wa marehemu baada ya kufanyiwa uchunguzi tayari umekabidhiwa kwa ndugu ili kuendelea na taratibu za mazishi.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa wa Majengo, Yohana Mapembe, alisema tukio hilo wamelipokea kwa masikitiko makubwa kutokana na kijana huyo mhitimu wa chuo cha ualimu mwaka 2019, kutojihusisha na matukio ya ovyo.

"Kitumbo ni kijana ambaye alikuwa wa mfano kwa vijana wengi. Baada ya kuhitimu Chuo cha Ualimu Singida mwaka 2019 alikuwa anajishughulisha na ufundi pikipiki katika Kata ya Ichenjezya mjini Vwawa," alisema Mapembe.

Kaka wa marehemu, Reagan Kitumbo, alisema mdogo wake alionekana kuwa na homa kidogo kwa muda mfupi, lakini hakuwa na tatizo lingine lolote kipindi hicho chote, jambo lililowaumiza baada ya kuukuta mwili juu ya mti.



Mkazi wa Kijiji cha Maturi, Kata ya Mnadani, jijini Dodoma, Athuman Juma, akichota maji yasiyo salama kwenye kisima kwa ajili ya matumizi ya nyumbani juzi, alidai kuwa kutokana na uhaba huo wamekuwa wakitumia maji hayo pamoja na mifugo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wakili wa bosi wa zamani NIDA ajitoa

**Na Kulwa Mzee**

WAKILI, Joseph Ndunguru aliyekuwa akimtetea Mkurugenzi wa zamani wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Dickson Maimu na Mkurugenzi wa Sheria, Sabina Raymond, amejitoa kuwawakilisha washtakiwa hao.

Hayo yalibainika jana Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashid Chaungu, wakati kesi hiyo ilipokuja, kwa ajili ya washtakiwa kuanza kujitetea.

Wakili Sosthenes Mbedule, anayemwakilisha mshtakiwa wa pili, alidai washtakiwa walitakiwa kuanza kujitetea, lakini mshtakiwa wa kwanza na mshtakiwa wa pili hawana wakili baada ya kuandika barua ya kujitoa.

Maimu alipoulizwa kama ana taarifa na wakili wake, alidai alipata taarifa hizo Ijumaa, lakini hajaonana naye na kuomba kupewa muda wa kutafuta mwingine.

Mshtakiwa Maimu anadai aliomba kupewa mwenendo wa kesi, lakini hawajapewa.

Wakili wa Serikali Kuu, Zakaria Ndaskoi, alidai upande wa Jamhuri walikuwa tayari kuendelea, hawakuwa na pingamizi kwa maombi ya washtakiwa, wapewe mwenendo wa kesi ndani ya muda mfupi, ili kesi iendelee.

Alidai hoja ya mshtakiwa wa kwanza na watano kutafuta wakili ni haki yao kisheria, aliomba shauri hilo lipangwe kwa kutajwa, ili kutoa fursa ya kupata nakala za mwenendo wa kesi na wapate nafasi ya kutafuta wakili.

Hakimu Shaungu baada ya kusikiliza hoja zote alisema mwenendo wa kesi unachapwa ukiwa tayari watapewa.

"Baada ya wiki mbili tukikutana ndiyo tutapanga tarehe ya kuanza utetezi, mahakama inawapa muda wa kutafuta wakili, mkipata kabla ya tarehe ya kutajwa si vibaya akaja kufuatilia mwenendo wa shauri," alisema Hakimu.

Mawakili wengine wa utetezi ni Tuli Kaundime na James Mwenda.

Mahakama iliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 8, mwaka huu.

Maimu anatarajia kuwa na mashahidi si chini ya 20 na vielelezo visivyozidi 10 wakati wa utetezi.

Hakimu Chaungu alisema amepitia ushahidi na vielelezo vilivyowasilishwa mahakamani na upande wa mashtaka na aliridhika kuwa washtakiwa wote wana kesi ya kujibu na wanatakiwa kujitetea.

Katika kesi hiyo, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 55 likiwamo la kuongoza genge la uhalifu, kughushi, kutoa nyaraka za kughushi kwa lengo la kumdanganya mwajiri, kusababisha hasara, utakatishaji fedha na matumizi mabaya ya madaraka.

Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka ulikuwa na jumla ya mashahidi 26 pamoja na vielelezo 45.

Mbali ya Maimu, washtakiwa wengine ni aliyekuwa Mkurugenzi wa Sheria Sabina Raymond, Xavery Kayombo, Meneja Biashara wa (NIDA), Aveln Momburi, na George Ntalima.

Maimu na wenzake wanakabiliwa na mashtaka mbalimbali likiwamo kuisababishia hasara serikali Sh. bilioni 1.175.

# Wataka somo la demokrasia

**Na Mwandishi wetu**

WADAU wa elimu, wameishauri serikali kuingiza somo la demokrasia kwenye mitaala ya shule za msingi ili kuwajengea uelewa wanafunzi kwenye masuala hayo tangu wakiwa wadogo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kitabu cha Kiini cha Demokrasia kilichoandikwa na Eamon Butler, Mshauri wa Wanafunzi Msaidizi kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Michael Stephano, alisema demokrasia ni mfumo bora lakini baadhi ya watu hawatambui jinsi unavyofanya kazi.

Stephano alisema kutokana na changamoto hiyo upo ulazima wa watu hasa wanafunzi kufundishwa tangu wakiwa wadogo, ili kuuelewa mfumo wa demokrasia unafanyaje kazi na unatekelezwaje.

Naye Mhadhili kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Dk. Tatu Nyange, alisema demokrasia ni pana hivyo ni ngumu wananchi kuelewa kwa urahisi kwa sasa.

"Ndiyo maana tunashauri kuwa liwapo somo la demokrasia ngazi ya shule ya msingi ili kuotesha mizizi ambayo itasaidia kuwa na idadi kubwa ya Watanzania wanaoelewa neno demokrasia kwa upana.

Ni wazi kuwa demokrasia ina faida na hasara zake, hivyo somo hili likifundishwa kuanzia ngazi ya chini litasaidia kuwapo kwa uelewa mpana," alisema Dk. Nyange.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Kisera na Elimu ya Liberty Spark, Evans Exaud, alisema uzinduzi wa kitabu hicho umelenga kutoa uelewa mpana kwa jamii juu ya maana halisi ya demokrasia.

"Kitabu hichi kimeeleza kiundani dhamira kuu iliyopo ndani ya demokrasia na kujikita kueleza aina zote tatu za demokrasia ambazo ni kisiasa, kijamii na kiuchumi. Kupitia kitabu hiki mwandishi ameeleza kiundani maana halisi ya demokrasia na kuweka wazi kila nchi duniani ina demokrasia yake kutokana na jamii iliyopo na utamaduni wake," alibainisha.

**"Ndiyo maana tunashauri kuwa liwapo somo la demokrasia ngazi ya shule ya msingi ili kuotesha mizizi ambayo itasaidia kuwa na idadi kubwa ya Watanzania wanaoelewa neno demokrasia kwa upana.**

# Polisi, LSF wakubaliana kukuza haki

**Na Frank Monyo**

JESHI la Polisi limezindua mwongozo wa jumla wa utendaji kazi (Police General Order) baada ya kuufanyia marekebisho yanayolenga kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa jeshi hilo.

Marekebisho ya mwongozo huo yalizinduliwa jana jijini Dar es Salaam na Mkuu wa Jeshi hilo (IGP) Simon Sirro.

Kutokana na uhitaji wa maboresho ya mwongozo huo, jeshi hilo limeingia makubaliano na shirika lisilo la kiserikali linalofanya kazi ya kukuza upatikanaji wa haki nchini la Legal Services Facility (LSF).

LSF lilitoa Sh. milioni 400 kwa ajili ya kuendesha mchakato mzima wa kupitia upya mwongozo uliokuwapo awali na kuangalia maeneo ambayo yanaweza kuboreshwa zaidi ili kuendelea kulinda na kutetea haki za wanawake na watoto nchini.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa mwongozo huo, IGP Sirro alisema anayo furaha kushirikiana na LSF katika kufanikisha kupitia na kurekebisha mwongozo wa Jeshi la Polisi nchini, ambao sasa utasaidia kuwalinda zaidi wanawake na watoto kama kundi maalum linalohitaji uangalizi kutokana na kuathirika zaidi na vitendo vya ukatili.

"Kutokana na kushamiri kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia nchini, ilitulazimu kuanzisha madawati maalum ya jinsia na watoto ndani ya jeshi letu ili kushughulikia tatizo hili.

"Uundwaji wa madawati haya ulikuwa jitihada mahususi za kiu ya kutaka kuwalinda wanawake na watoto dhidi ya ukatili mbalimbali ingawaje madawati haya hayakuwa yameingizwa rasmi katika Amri ya Jumla ya Jeshi la Polisi au Mwongozo wa Jumla wa Utendaji wa Jeshi la Polisi," alifafanua.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema kukamilika kwa mapitio na maboresho ya mwongozo wa jeshi hilo ili kusimika ama kutambua rasmi jitihada zilizokuwapo kama vile madawati ya jinsia na mtandao wa askari wanawake ndani ya jeshi hilo, ni sehemu ya mkakati maalum wa LSF kushirikiana na serikali pamoja na taasisi zake katika kufanya uchechemuzi, ili kuleta mabadiliko ya kisera, sheria na miongozo mbalimbali nchini.

"Uzinduzi huu una maana kubwa sana kwetu kama shirika binafsi linalofanya kazi ya kukuza upatikanaji wa haki nchini Tanzania.

"Hii ni sehemu ya ushirikiano wetu na Jeshi la Polisi kupitia makubaliano tuliyotiliana saini ili kusaidia kuupitia upya mwongozo wao ili kurasimisha kabisa madawati ya jinsia, ambayo yamekuwa yakifanya kazi kubwa ya kulinda na kutetea haki za wanawake na watoto nchini," alisema.

Akinukuu ripoti ya LSF ya mwaka 2020, N'wanakilala alisema inaonyesha takribani watu 99,844 walipatiwa huduma za msaada wa kisheria nchi nzima. Kati yao, wanawake walikuwa 60,203 sawa na asilimia 60 na wanaume 39,641 sawa na asilimia 40.

"Ripoti yetu inaonyesha katika kila matukio manne ya ukatili yaliyoripotiwa na wanawake, yalihusisha unyanyasaji wa kijinsia, ambapo visa vyote vilivyoripotiwa vinakadiriwa kufikia asilimia 26.5 kwa mwaka 2020," alibainisha.

# Taasisi ya Mkapa yatia mkono kukabili corona

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Benjamin Mkapa katika kuiunga mkono serikali kukabiliana na tatizo la upungufu wa watumishi wa afya hasa kipindi hiki cha corona, imeajiri watu 3,195 ili wasaidie utoaji wa huduma za afya zikiwamo za chanjo katika mikoa 20 nchini.

Mkurugenzi wa Miradi wa taasisi hiyo, Rahel Sheiza, alisema jana mkoani Dar es Salaam kuwa wameajiri watumishi 605 katika mikoa 20 yenye vituo vya kutolea huduma na wengine 2,590 wanaotoa huduma ya elimu ya afya ngazi ya jamii.

Alibainisha hayo wakati wa mkutano baina yao na wahariri na waandishi wa habari waliokutana kujadili matatizo ya uhaba wa watumishi katika Sekta ya Afya na namna bora ya kukabiliana nayo.

Alisema taasisi hiyo imekuja na mkakati wake unaoendana na mkakati wa kitaifa wa chanjo na ule wa kuboresha huduma za afya katika ngazi za vituo, lengo ni kwamba wanapohamasisha watu wachanje, lazima wahamasishe wajikinge.

"Tunatoa elimu kuongeza nguvu kwenye kuchanja, kuwajengea uwezo watumishi wa afya kuhusu kutoa huduma ya kuchanja, watumishi wetu wa afya ngazi ya jamii wanaendelea kuelimisha makundi maalum yenye kipaumbele," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema watoa huduma wa afya ngazi ya jamii wanafuatilia watu wanaopewa vipaumbele katika chanjo na kupata mrejesho na kurudisha kwa wataalamu wa afya ili kufanya uchambuzi kuhakikisha zinaendelea kutolewa kwa njia salama.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Dk. Ellen Senkoro, alisema taasisi hiyo inatambua Sekta ya Afya ina kazi kubwa ya kufanya kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya njema ili kufikia Malengo ya Milenia na ya kitaifa.

"Miradi mingi ya Taasisi ya Mkapa imejikita katika kuimarisha mifumo afya. Sekta hii inahitaji rasilimali watu, tunapenda na ninyi muwe wadau wakubwa kuongeza chachu ya uwekezaji wa rasilimali watu Sekta ya Afya," alisema.

Dk. Senkoro alibainisha bado kuna tatizo la upungufu wa watumishi katika sekta hiyo, akitaja uhitaji wa watumishi takriban 200,000, lakini waliopo ni asilimia 48 (takwimu halisi takriban 98,000), hivyo wanaohitajika ni zaidi ya 100,000.

"Huu upungufu ndiyo tunataka tuangalie tunafanyaje kuziba hili pengo la asilimia 52 zilizobaki.

"Viwango vya Shirika la Afya Duniani (WHO) vinasema angalau kuwe na daktari mmoja kati ya watu 1,000 lakini tuna daktari mmoja kwa watu 20,000," alilalamika.

Pia alisema upo utofauti mkubwa kati ya maeneo ya mjini na vijijini, akibainisha kuwa vijijini uwiano ulipo ni daktari mmoja kwa watu 78,000 na mjini ni daktari mmoja kwa watu 9,000.

"Taasisi yetu haikusimama nyumba wakati wa mlipuko wa COVID-19, tuliona watumishi ni wachache na mahitaji ni makubwa.

"Tuliongeza watumishi wa afya sio tu kwenye vituo vya afya, (bali) hata kwenye maeneo ya mipaka ya nchi. Hata sasa katika suala la chanjo tunashirikiana na serikali ili kuhakikisha idadi ya watu wanaotakiwa kupata chanjo inaongezeka," alisema.




Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Simon Sirro, akimkabidhi Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Legal Services Facility (LSF), Lulu Ng'wanakilala, tuzo ya heshima kwa kudhamini zoezi zima la kufanya mapitio ya Mwongozo wa Jumla wa Utendaji Kazi wa Jeshi la Polisi (Police General Orders), uliokamilika na kuzinduliwa rasmi jijini Dar es Saalam jana. Kulia ni Meneja wa Mawasiliano LSF, Jane Matinde. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Timu yaundwa kupitia mifumo ya kodi

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imeunda timu ya wataalamu 10 watakaopitia mfumo wa ukusanyaji mapato na matumizi ya serikali, kupendekeza namna ya kuboresha kodi zinazotozwa ili kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji wa biashara hapa nchini.

Akizindua timu hiyo jana jijini Dar es Salaam yenye wajumbe wabobezi katika masuala ya uchumi, kodi, fedha na mifumo ya matumizi ya serikali, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema watakwenda kufanya tathmini na kutoa mapendekezo kwa serikali juu na namna bora ya ukusanyaji mapato kutakakoendana na ukuaji wa uchumi.

"Ni imani yangu kuwa timu hii ninayoizindua leo kwa miezi sita itakuja na mapendekezo yatakayoboresha mfumo uliopo pamoja na kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na matumizi ya serikali, hivyo kuwa na bajeti endelevu," alisema Dk. Nchemba.

Alisema sehemu ya majukumu mahsusi ya timu hiyo ni pamoja na kufanya tathmini ya mfumo wa kibajeti na kupendekeza namna bora ya kuiwezesha serikali kuwa na bajeti endelevu.

Jukumu lingine ni kufanya ulinganishi wa mfumo wa kodi wa Tanzania na nchi nyingine zinazofanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Dk. Mwigulu alitaja jukumu lingine ni kupitia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya mifuko yenye vyanzo maalum na kushauri ipasavyo iwapo kuna haja ya kuendelea nayo au vinginevyo kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa bajeti ya serikali.

Alitaja jukumu lingine ni kufanya tathmini ya mwenendo wa nakisi ya bajeti ya serikali na kutoa mapendekezo kwa kuzingatia mahitaji muhimu ya serikali.

Alisema timu hiyo itafanya tathmini ya ukuaji na ugharamiaji wa deni la serikali, ulipaji wa mishahara, ulipaji wa malimbikizo ya madai/madeni na ukuaji wake.

Kadhalika, alitaja jukumu lingine kuwa ni kupitia gharama, taratibu za uanzishaji na uendeshaji wa biashara nchini na kupendekeza namna ya kuboresha kodi zinazotozwa ili kuweka mazingira wezeshi ya ufanyaji wa biashara hapa nchini.

Dk. Nchemba alisema wastani wa ukusanyaji wa kodi katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ni asilimia 15.1 ya Pato la Taifa, wakati kwa nchi zilizoendelea zinakusanya hadi asilimia 40 ya pato la taifa au zaidi, kwamba kiwango hicho kinaziwezesha nchi zilizoendelea kugharamia kikamilifu matumizi muhimu ya kiuchumi na kijamii.

Alisema hata hivyo kiwango cha ukusanyaji wa mapato ya kodi nchini ni chini ya wastani wa ukusanyaji wa kodi katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Dk. Mwigulu alisema: "Kwa mfano mwaka 2020/21, jumla ya mapato ya ndani yalikuwa asilimia 13.3 ya pato la taifa, mapato ya kodi yalichangia asilimia 11.2 ya pato la taifa."

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni wakati mwafaka NEC kuwa na ofisi, watumishi majimboni

**KWA** kipindi kirefu yamekuwapo mapendekezo kutoka kwa wadau kutaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuwa na ofisi na watumishi wake hadi ngazi ya majimbo.

Lengo limekuwa likielezwa kuwa ni kuifanya NEC kuwa chombo huru katika kutekeleza jukumu lake la kikatiba la kuandaa, kuratibu na kusimamia uchaguzi kwa tija na ufanisi.

Tangu kuanzishwa kwa NEC mwaka 1992 baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa, imekuwa ikikosolewa kutokana na jinsi inavyotekeleza jukumu lake la msingi na la kikatiba.

Malalamiko mengi ya wadau yamekuwa yakielekezwa katika suala la kutokuwa na ofisi zake wala watumishi wake kwenye wilaya na majimbo, hivyo kutekeleza majukumu yake kwa kutumia wakala ambaye ni wakurugenzi wa halmashauri za miji, wilaya, nanispaa na majiji.

Wakurugenzi hao amekuwa wakikosolewa kutekeleza majukumu ya NEC kwa madai kwamba hawawezi kutoa haki kwa sababu ni waajiriwa wa serikali, ambao hawatokani na chombo huru.

Pamoja na kuwapo malalamiko hayo na mapendekezo ya wadau kwa muda mrefu, jambo hili halijafanyiwa kazi na matokeo yake ni kuwa hivi karibuni zimeonekana dosari na kasoro kubwa katika usimamizi wa uchaguzi mbalimbali.

Miongoni mwa dosari hizo ni wakurugenzi kuwaengua wagombea wengi wa vyama vya upinzani wakati wa uteuzi kwa maelezo ya kukosea kujaza fomu, mawakala wa vyama hivyo kutoruhusiwa kuingia katika vituo vya kupigia kura na wakati mwingine kuchelewa kuruhusiwa. Pia wakurugenzi wamekuwa wakilalamikiwa kuondoka ofisini, hivyo, wagombea wa upinzani kushindwa kurejesha fomu.

Malalamiko haya tunaona kwamba sasa ni wakati mwafaka kutafutiwa ufumbuzi, kubwa zaidi ni NEC kuwa na watumishi na ofisi zake ngazi ya wilaya/majimboni, hivyo kuacha kuwatumia wakurugenzi, ambao wanategemea maelekezo ya mamlaka ya uteuzi.

Mwenyekiti mstaafu wa NEC, Jaji Damian Kubuva, akiwa kwenye wadhifa huo kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, aliahidi kuwa tume ilikuwa na mpango wa kuwa na watumishi kuanzia makao makuu hadi wilayani ili kutekeleza majukumu yake yenyewe.

Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA) juzi ilisema kuwa NEC ikiwa na watendaji wake ngazi ya halmashauri, kasoro ambazo hujitokeza mara kwa mara katika uchaguzi zitapungua.

Moja ya kasoro zilizotajwa na CEGODETA ni tuhuma za kuwapo kwa baadhi ya mawakala wa vyama kunyimwa nakala za viapo kutokana na baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi katika ngazi hiyo kuwa ni makada wa chama tawala.


Taasisi hiyo ilisema inajua kwamba uchaguzi huwa unakumbwa na kasoro nyingi ikiwamo ya baadhi ya mawakala kunyimwa viapo, na kuwa hiyo inatokana baadhi ya wakurugenzi wa halmashauri ni makada.

Hata hivyo, tunaamini kuwa serikali imeshaliona hili, kutokana na kauli ya Rais Samia Suluhu Hassan wiki iliyopita wakati wa kupokea ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa 2020 kutoka NEC; kwa kutaka baadhi ya sheria kufanyiwa marekebisho.

Pamoja na mambo mengine, tunaona kuwa suala la NEC kuwa na ofisi kwenye wilaya/majimbo ni wakati mwafaka kufanyika sasa kwa lengo la kuendesha uchaguzi kwa njia za uhuru na haki pamoja na kuondoa malalamiko ya kila mara kuwa inapendelea chama kimoja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Ester Mgidula

# Vita Gwajima, Waziri Afya isichukuliwe poa

**JINA** la Mchungaji Josephat Gwajima na la Dk. Dorothy Gwajima, Waziri wa Afya, ndiyo yanayoshika kasi kwa sasa, kutokana na malumbano kati yao, ambayo mzizi wake ni chanjo ya corona.

Miaka ya nyuma, Gwajima, Mbunge wa Kawe (CCM) na Askofu wa Kanisa Ufufuo na Uzima alishawahi kuwa maarufu kutokana na mambo kadhaa ya kisiasa na kidini, safari hii anapata umaarufu kwenye afya kutokana na kupinga chanjo ya corona.

Licha ya kwamba ilianza kama utani baada ya Askofu Gwajima kutangaza msimamo wake dhidi ya chanjo ya corona, akidai kuwa hana mpango wa kuchanjwa na kuonya watu wasichanje, kauli yake ilizua taharuki na kupokelewa kwa hisia tofauti.

Wapo walioona kuwa anatafuta 'kiki' kama vijana wengi wa mjini wanavyosema, lakini muda ulivyosonga mbele ndivyo ambavyo ilionekana kuwa Askofu Gwajima amemaanisha kile alichokuwa akikizungumzia na ameendelea kukisimamia.

Huo ni msimamo wake na ana haki ya kutoa maoni yake, isipokuwa inachukuliwa tofauti kwa kuwa nguvu yake katika jamii ni kubwa na ana ushawishi mkubwa kutokana na imani na huduma zake kwa wanaomfuatilia.

Hatua ya Waziri Dorothy Gwajima kujibu hoja za Askofu Gwajima, akiingia katika masuala binafsi, inamaanisha kuwa aliupeleka mvutano huo katika hatua nyingine.

Binafsi naamini kuwa hoja iliyotakiwa kubaki ni kuhusu kuchanjwa na msimamo wake kama ambavyo Askofu Gwajima amekuwa akielezea hisia zake, lakini kuingia kwenye maisha binafsi hilo ni jambo jingine.

Mada hiyo ilienda mbele zaidi kwa kuhusisha mambo binafsi ya familia baada ya Askofu kutumia madhabahu kujibu hoja kwa kumtaja kaka yake halikuwa jambo la busara, kwa kuwa wahusika hao wana uhusiano wa kindugu.

Kibaya zaidi ni kuwa wakati wote ni wanachama na wabunge wa CCM, walikuwa na nafasi ya kubishana hoja kwa hoja ndani ya vikao vyao, lakini kuingiza masuala binafsi na ya kifamilia kwenye ibada na mitandao ya kijamii pengine haikuwa sawa.

Waziri ni kiongozi, ana heshima kitaifa , kauli yake anapoitoa popote inachukuliwa kama serikali, kwa upande wa Askofu Gwajima, heshima yake ni kubwa kwa waamini wake na wengine wanaomwamini na kumkubali kutokana na kuhubiri Injili.

Inajulikana wazi kuwa kunapokuwa na mgogoro wa kifamilia au lolote lenye utata uamuzi wake pia unahitaji busara na uvumilivu.

Kitendo cha wanasiasa hao kulifanya suala la chanjo ya virusi vya corona kama la kisiasa, utani au ajenda ya kulipua mambo ya watu binafsi naliona kama hailiko sawa.

Naamini serikali inatamani na itahakikisha idadi kubwa ya watu wanapata chanjo ili kuwakinga na ugonjwa huo, ni vema busara zikatumika katika kurejesha mambo kwenye mstari na mambo yakamalizika.

Chanjo ni hiari, ibaki hivyo labda kwa wale serikali itakaowaagiza kuwa ni lazima wachanjwe kutokana na majukumu yao, hivyo utani kama huo unaoendelea kipindi hiki usiwe na ulazima ili kila mmoja awe na uhuru wa kufikiria na kufanya uamuzi lakini akizingatia kuwa chanjo ni hiyari , lakini pia kujikinga na corona ni jambo jema.

Pengine viongozi wangetambua kuwa ni taa ya kuwaongoza Watanzania kwahiyo kama watazimika wananchi watajikuta wamekwama katika vikwazo na kukosa wa kuwasaidia.

Ninawomba kuacha mivutano isiyokuwa na sababu na ukweli ubaki kuwa chanjo ni hiari na wote mbunge na Waziri wa Afya mshirikiane kujenga taifa kama ambavyo, mmekuwa mkifanya siku zote.

Serikali imeshatangaza kuwa corona ipo na ina madhara na inaua, kwahiyo ni jukumu la kila mwananchi kuchagua upande anaoona upo sahihi, kwa kusikiliza na kutafakari mambo mbalimbali lakini mwisho, 'akili ya kuambiwa, changanya na yako'.

HABARI KITAIFA

## Kortini madai ya kumwibia mwajiri

**Na Waandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wanne wa Benki ya NBC Tawi la Mbagala, Dar es Salaam, wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za kumwibia mwajiri wao zaidi ya Sh. milioni 243.2.

Mbele ya Hakimu Mwandamizi Agustina Mmbando, Wakili wa Serikali Adolf Verandumi, alidai watuhumiwa hao walitenda kosa hilo kwa nyakati tofauti mwaka 2018.

Watuhumiwa hao ni Grace Jonah (50), Rahma Mkumba (36), Ahmed Khalidi (34) na Patrick Chimotto (53) wote wakazi wa Dar es Salaam.

Wakili Verandumi alidai kuwa Machi 3, 2018 na Aprili 30, 2018 washtakiwa hao waliiba Sh. 243,270,550 mali ya mwajiri wao, Benki ya NBC. Washtakiwa wote wanne walikana mashtaka hayo.

Baada ya kukana mashtaka, upande wa utetezi uliomba mahakama hiyo kutoa dhamana kwa washtakiwa hao.

Hakimu Mbando alikubali ombi hilo na kutoa masharti ya dhamana kwa kila mshtakiwa, kuwasilisha Sh. milioni 30 taslimu au mali isiyohamishika yenye thamani hiyo.

Pia kila mmoja alitakiwa kuwa na barua mbili za wadhamini zenye picha mbili pamoja na vitambulisho vya kazi na taifa na kuwasilisha hati zao za kusafiria mahakamani.

Wakili wa serikali alidai mahakamani kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

***Imeandikwa na Beatrice Inyasi, Paulina Chimeledya na Kalebo Mussa (TUDARCo)***

# Bunge laiagiza TRA kesi za kodi ya tril. 360/-

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imeiagiza Mamlaka ya Mapato (TRA) kukamilisha kazi ya kujibu hoja za ukaguzi zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ifikapo Juni mwakani, ikiwamo kuzishughulikia kesi za kodi za Sh. trilioni 360.

Akizungumza na Nipashe baada ya kufanya mahojiano na TRA kuhusu hoja za ukaguzi zilizoibuliwa na CAG kwenye fedha za taifa, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, alisema hoja za ukaguzi zilikuwa 300, lakini 66 ndio zimefanyiwa kazi.

Aidha, alisema kutoshughulikiwa kwa kesi hizo ikiwamo ya makinikia kunatokana na tatizo la kuchelewa kuundwa bodi za rufani mapema na Wizara ya Fedha na Mipango.

"Wizara ya Fedha ndio inayounda bodi ina mwenyekiti, lakini haina wajumbe wa bodi, kwa hiyo hizo bodi hazikai kwa wakati na matokeo yake kunakuwa na malimbikizo makubwa ya kodi. Kwa mfano, ile kesi ya kikodi ya makinikia haijashughulikiwa na unakuta kodi zingine zinadaiwa tangu mwaka 2001 mpaka leo miaka 20, sasa kodi gani miaka 20 itakuwa na thamani kweli?" Alihoji. Alieleza kuwa kama kuna kesi zingine zimeshafungwa, serikali iombe zifutwe na kuondokana na malimbikizo ya hoja ambazo zinaonyesha madeni makubwa ya kodi yasiyo na maana.

"Tumewaambia kabla ya Juni waje tena tuangalie wamefikia wapi ukamilishaji wa madeni yote ya kodi yanayodaiwa, waende kuangalia namna ya kumaliza hili, hili ni tatizo hatuwezi kuzungumzia hilo miaka nenda rudi," alisema.

Kadhalika, Kaboyoka alisema TRA imeagizwa kutokadiria wananchi kodi kubwa na kusababisha kufunga biashara.

"Tunataka makadirio yawe ya kweli yasiyo yale ya kumkomoa mwananchi na kusababisha kufunga biashara," alisema.

Pia alisema kamati iliagiza TRA kutazama mifumo yao.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Japhet Hasunga, alisema TRA inatakiwa kuzifanyia kazi hoja hizo na kuzifunga kwa kuwa nyingi ni za muda mrefu.

"Tunataka bodi ziundwe maana zingine hazina wajumbe wakutosha ufanyaji kazi wa zile bodi imekuwa ni changamoto, matrilioni ya fedha yanaonekana zipo mkononi mwa watu, kutokana na kesi zao hazijaisha, tunataka bodi zile zifanye kazi ziwezeshwe ili kumaliza hayo mambo," alisema.

"Kuna kesi zinatokana na wale watu wanaosafirisha mizigo, ambao wanasema inaenda on transit, lakini ikifika mwisho haitoki... sasa kuna kodi inatakiwa sasa ilipwe baada ya kuikamata hiyo mizigo yaani wanaishusha ndani badala ya kutoa nje wakati wamesema inaenda kwenye on transit."

"Lakini kuna mafuta ambayo wanathibitisha kuwa inaenda on transit halafu mafuta yanashushwa humu ndani, kuna mengine yanashushwa humu ndani wanalipa kodi kama kawaida sasa zile taarifa kwenda kwenye mfumo kwa kuzifuta kuwa tayari kesi imekwisha hazifutwi, inaonekana zinakwenda on transit hoja haijafungwa na kumbe walishalipa," alisema.

Alifafanua suala la makinikia lipo kwenye kesi za kodi ambazo za Sh. trilioni 360, na kwamba kama suala lilishaisha lifutwe kuliko kuonekana zinadaiwa wakati hazidaiwi.



Madiwani Manispaa ya Shinyanga, wakiushusha kaburini mwili wa aliyekuwa Meya wa Manispaa hiyo, marehemu David Nkulila, wakati wa mazishi yake yaliyofanyika kwenye makaburi ya Dodoma mjini Shinyanga jana. Nkulila, alifariki dunia Agosti 23, mwaka huu kwa ugonjwa wa moyo. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Vijana wahimizwa matumizi ya teknolojia

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imesema imeweka mazingira wezeshi ya kuendeleza na kufanikisha matumizi ya TEHAMA nchini, huku ikiwahimiza vijana kutumia teknolojia hiyo katika kuchangamkia fursa zilizopo katika sekta ya mawasiliano.

Hayo yalibainishwa jana jijini Dar es Salaam na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mulembwa Munaku, wakati akifungua kongamano la kidijitali la vijana nchini kwa niaba ya Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Faustine Ndugulile.

Alisema wizara hiyo imetengeneza sera ya taifa ya TEHAMA, sheria na kanuni, ujenzi wa miundombinu ya TEHAMA ikiwamo mkonga wa taifa wa mawasiliano wenye urefu wa kilomita 8,319 unaofikisha huduma za mawasiliano kwenye mikoa na nchi jirani.

"Zaidi ya asilimia 75 ya Watanzania ni vijana na serikali imetambua hilo, hivyo imeweka mikakati na miradi ya TEHAMA inayogusa vijana ili kuongeza wigo wa fursa ya teknolojia hiyo katika nyanja mbalimbali ikiwamo fursa ya ajira, biashara, mafunzo na ubunifu, ili itumike kutatua na kujibu changamoto zinazoikabili jamii.

"Katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka huu, serikali imepata mkopo nafuu wa dola za Marekani milioni 150 kutoka Benki ya Dunia ili kutekeleza mradi wa Tanzania ya Kidijitali na mradi huo utagusa vijana na TEHAMA katika nyanja ya kiuchumi na kijamii," alisema Munaku.

Naibu kiongozi wa ujumbe wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini, Emilio Rossetti, alisema kupitia umoja wao wamekuwa wakitoa misaada nchini na kushirikiana na serikali kuendeleza na kuongeza matumizi ya TEHAMA.

"Tumeshirikiana na serikali kuongeza matumizi ya TEHAMA husuan kwa vijana na wanawake na tuko tayari kuendelea kufanya hivyo ili vijana wanufaike na fursa zinazotokana na teknolojia hiyo," alisema Rossetti.

Mkurugenzi Mkazi wa Kampuni ya DOT Tanzania, Diana Ninsiima, alisema kampuni hiyo imeshirikiana na wadau wengine kuandaa kongamano hilo ili litumike kama jukwaa la kujenga uelewa kwa jamii kuhusu nafasi ya vijana katika TEHAMA ikiwa na kauli mbiu 'Ujuzi wa Kidijitali kwa ajili ya Ajira na Ujasiriamali kwa Vijana'.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Mtabe Innovations, Given Edward, akizungumza kwa niaba ya vijana, alisema kwa sasa vijana wa kitanzania wanapata mazingira sawa na vijana wengine duniani kutumia TEHAMA kuendesha maisha yao na wanaishukuru serikali kwa kubadilisha mitazamo ya jamii kuhusu umuhimu na manufaa ya teknolojia hiyo.

Katika kongamano hilo walihudhuria wadau mbalimbali kama Umoja wa Mawasiliano Duniani, Ofisi za ubalozi wa Canada, Ireland, UNICEF, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, na kampuni za TEHAMA za vijana zilizopo nchini.

# Wadai kuchangishwa mafuta ili kupata huduma ya upasuaji

**Na Julieth Mkireri**, RUFIJI

WAKAZI wa Kijiji cha Nyaminywili, Rufiji mkoani Pwani, wameiomba Serikali kuwasaidia upatikanaji wa huduma ya upasuaji katika kituo cha afya kilichoko kijijini hapo.

Wakizungumza na Nipashe juzi, baadhi ya wanawake wa kijiji hicho walisema kukosekana kwa huduma hiyo kumekuwa tatizo, hivyo kusababisha kuchangia fedha za mafuta lita 25 hadi 30 kwa ajili ya gari la wagonjwa kwenda kupata huduma hiyo katika hospitali zingine.

Pilly Magawa, mmoja wa wakazi hao, alisema inapotokea mmoja wao anahitaji huduma ya upasuaji, analazimika kusafirishwa hadi Hospitali ya Utete ambako huduma hiyo inapatikana.

Naye Halima Mussa alisema kutokana na tatizo hilo, baadhi ya wanawake wamepoteza maisha wakati wakipelekwa kupatiwa huduma ya upasuaji.

Alisema chumba cha huduma hiyo katika kituo cha afya kijijini hapo kimekamilika muda mrefu lakini hakijaanza kutoa huduma.

Mussa alisema baadhi ya wanawake wanapokaribia kujifungua, wenye ndugu mjini wanalazimika kwenda huko hadi pale watakapojifungua ili kupata urahisi wakati unapofika.

"Unapokaribia kujifungua wanakwambia mapema utayarishe fedha ya mafuta kukufikisha Utete au Songa ambako utapata huduma ya upasuaji. Unalazimika kufanya jitihada hata kukopa kutokana na hali zetu za kimaisha ili ikitokea dharura uwahishwe," alisema Mariam Amiri, mkazi mwingine wa kijiji hicho.

Mganga Mfawidhi wa Kituo hicho, Dk. William Ismail, alikiri kukamilika kwa ujenzi wa chumba cha upasuaji kwa muda mrefu na kwamba kwa sasa vifaa vyote tayari vimefungwa kwa ajili ya kutoa huduma hiyo.

Ismail alisema vifaa hivyo vimefungwa mwezi uliopita na kwamba kwa sasa bado hajapatikana mgonjwa anayetakiwa kupatiwa huduma hiyo.

Kuhusu fedha za kuchangia mafuta, mganga huyo alikiri na kusema hiyo ni kutokana na ufinyu wa bajeti, hivyo anayetumia gari la wagonjwa anatakiwa kuchangia mafuta kulingana na umbali.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na wanachama wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU), alipofungua Mkutano Mkuu wa chama hicho, jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Wajasiriamali, wamiliki viwanda watakiwa kupata alama za ubora

**Na Mwandishi Wetu**, LIWALE

WAJASIRIAMALI na wenye viwanda Liwale mkoani Lindi, wametakiwa kujitokeza katika ofisi za Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kupata alama za ubora, hatua ambayo itawawezesha kuondokana na vikwazo vya kibiashara na kupanua wigo wa soko la bidhaa zao.

Wito huo ulitolewa kwa nyakati tofauti juzi na jana na maofisa wa TBS, walipowatembelea wajasiriamali na wenye viwanda na kuzungumza nao katika maeneo yao ya biashara kwa lengo la kuwahamasisha wajitokeze kupata alama ya ubora.

Akizungumza na waandishi wa habari wilayani hapa jana, Ofisa Usalama wa Chakula wa TBS, Barnabas Jacob, alisema wako wilayani Liwale kwa ajili ya kazi hiyo pamoja na kufanya ukaguzi.

"Kwa hiyo tunatoa wito kwa wajasiriamali kujitokeza kwa wingi kuthibitisha ubora wa bidhaa zao TBS hatua itakayowezesha bidhaa zao kuondokana na vikwazo vya kibiashara," alisema Jacob.

Alisema wanachotakiwa kuwa nacho ni barua ya utambulisho kutoka SIDO na baada ya hapo wakifika TBS mchakato unaanza mara moja, hivyo ni muhimu kwao kuchangamkia fursa hiyo.

Jacob alifafanua kwamba alama ya ubora kwa wajasiriamali inatolewa kwao bure na shirika hilo, kwani gharama zote zinalipwa na Serikali, hivyo wanachotakiwa wao ni kupitia SIDO kwa ajili ya kupata barua ya utambulisho.

Pia Jacob alisema wamefanya ukaguzi wa awali kwa wenye viwanda ambavyo wazalishaji wake wanataka kupata alama ya ubora.

Alitaja miongoni mwa viwanda ambavyo maofisa hao wa TBS wamefanya ukaguzi na kuhamasisha kujitokeza kupata alama ya ubora kuwa ni pamoja na vile vinavyokamua mafuta ya alizeti, viwanda vya kubangua korosho, kwenye mashine za kusaga unga pamoja na kiwanda cha uzalishaji wa bidhaa za mikate.

"Wote hao tumewafikia na kuwahamasisha kuja kupata alama ya ubora TBS," alisema Jacob.

Pia alitaja kazi nyingine ambayo wameifanya wilayani humo kuwa ni pamoja na kukagua na kusajili maduka ya vipodozi na chakula ili kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa kukidhi matakwa ya sheria za nchi na kulinda afya za watumiaji.

Alisema usajili majengo ya biashara unawapa wafanyabiashara uhakika wa kutunza bidhaa na kwamba wanasajili jengo kulingana na bidhaa zinazoenda kuhifadhiwa humo.

Usajili wa bidhaa, majengo ya vyakula na vipodozi ni takwa la kisheria ili kuwawezesha wafanyabiashara kufanya biashara bila vikwazo.

# Fukwe za Dar sasa kuonekana kivingine

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI imetangaza mpango wa kuziboresha fukwe zote katika Mkoa wa Dar es Salaam na kuzifanya za kisasa, sambamba na kuwawekea mazingira rafiki wafanyabiashara katika maeneo hayo.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, alisema hayo jana alipotembelea ufukwe wa Coco ili kujionea hali halisi katika eneo hilo na kuahidi maboresho ya kuufanya uwe wa kisasa na kwamba maboresho hayo yataanza muda wowote kuanzia sasa.

Pia alibainisha kwamba serikali imejizatiti kuziboresha fukwe zingine na kuzifanya kuwa sehemu ya utalii, burudani na mapumziko.

Katika kufanya hivyo, alisema amepata wadau ambao wamekubali kuwajengea vibanda vya kisasa wafanyabiashara katika ufukwe huo vitakavyosaidia eneo hilo kuwa na mandhari safi na nzuri.

"Nimekagua ufukwe huu nikiambatana na viongozi na wadau waliokubali kushirikiana na serikali katika maboresho ya fukwe wakiwemo benki za NMB, CRDB, kampuni za utengenezaji wa vinywaji zikiwemo TBL, Coca-Cola, Pepsi, Asas na Azam. Wote tutashirikiana katika kuzifanya fukwe kuwa za kisasa," alisema.

"Dhamira ya serikali ni kuona Coco inakuwa ya kisasa na shughuli za kiutalii zinafanyika. Tayari tumezungumza na mfanyabiashara mkubwa nchini, Said Salim Bakhresa, kwa ajili ya kuleta boti za utalii kwenye ufukwe huu," aliongeza.

Katika hatua nyingine, Makalla aliitaka Manispaa ya Kinondoni kupitia Mkuu wa Wilaya hiyo, Godwin Gondwe, kuanza mara moja ujenzi wa ofisi, stoo na vyoo vya kisasa kwenye ufukwe huo.

Sambamba na hilo, alitaka kupelekwa umeme katika eneo lote la Coco huku akimwelekeza Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kinondoni, Ramadhani Kingai, kuimarisha ulinzi na usalama.

Mpango wa kuboresha fukwe za Dar es Salaam unakwenda sambamba na maboresho ya maeneo ya wazi, bustani za kupumzika, usafi na upandaji miti na maua katika kingo za fukwe na pembezoni mwa barabara.

HABARI KITAIFA

# Watishia kugoma ununuzi wa dengu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAFANYABIASHARA mkoani Shinyanga wametishia kugoma kununua zao la dengu, kutoka kwa mkulima kutokana na masharti magumu ya serikali yanayowataka wasisafirishe zao hilo nje ya mkoa huo badala yake wauzie Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS).

Wamedai wananunua dengu kutoka kwa mkulima kwa Sh. 1,200 kwa kilo, lakini wakiuza kwenye AMCOS kwa mfumo wa stakabadhi ghalani bei yake ni Sh. 900 na kuwa wakifanya hivyo watapata hasara.

Wafanyabiashara hao wakizungumza juzi na Nipashe kwa masharti ya kutotajwa majina yao, walisema awali serikali iliwazuia wasinunue zao hilo kwa mkulima, baada ya kulalamika wakaruhusiwa, lakini limejitokeza katazo lingine la kutosafirisha dengu nje ya Mkoa wa Shinyanga, badala yake wauze kwenye AMCOS.

Aidha, walimwomba Rais Samia Suluhu Hassani, kuingilia kati suala hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, alitolea ufafanuzi suala hilo kuwa mazao hayo kwa mwongozo wa serikali, yanatakiwa yauzwe kwa mnada wa soko la bidhaa Tanzania TMX kwa mfumo wa stakabadhi ghalani kupitia AMCOS.

Alisema wakiuza mazao hayo kwa mfumo huo, AMCOS zitapata pia ushuru na halmashauri na kubainisha kuwa wafanyabiashara wanawaumiza wakulima na kudhoofisha halmashauri na ushirika, na kutolea mfano mwaka jana kupitia mfumo wa TMX zao la choroko kilo moja ilikuwa Sh. 1,600 na dengu Sh. 5,000.

# Ukosefu zahanati watesa wanavijiji

**Na Restuta Damian,** MULEBA

WAKAZI wa vijiji vitatu katika kata za Bihanga na Burungura wilayani Muleba mkoani Kagera hawana zahanati, hali inayowafanya kutembea kilomita 12 kutafuta huduma hiyo maeneo ya jirani.

Wakazi hao wanatoka katika vijiji vya Burungura na Kakoma ambao wanalazimika kutembea kwenda Kata ya Mubunda iliyopo jirani.

Mkazi wa kijiji cha Bihanga, Joanitha Kaijage, alisema ukosefu wa zahanati katika kijiji hicho umedumu tangu kijiji hicho kuanza, na kwamba wanawake wamekuwa wakipata shida ya kupata huduma hiyo.

Alisema wajawazito hujifungua njiani wakikimbizwa kwenye Kituo cha Afya cha Mubunda ambacho kipo kata jirani.

Mkazi mwingine wa Kijiji cha Burungura, Atugonza Rwija, alisema matukio ya kujifungulia njiani yamekuwa ni kawaida kwa kwa wanawake wengi wa kijiji hicho.

"Tunalazimika kujifungulia nyumbani ukiangalia umbali wa kutembea, lazima uzalie njiani muda mwingine hauna nauli ya pikipiki bado ukienda umeshajifungua wanakupiga faini ya kujifungulia nyumbani," alisema Kaijage.

Diwani wa Burungura, Dominick Domisian, alisema wanahamasisha ili wachangie fedha kwa ajili ya ujenzi wa zahanati.

Alisema katika kijiji cha Bihanga, wananchi wamejitolea kujenga msingi ambao tayari umekamilika na hatua inayofauta ni kupaua jengo hilo.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Dk. Deo Kusaka, alisema huduma katika vijiji hivyo hutolewa mara moja kwa wiki na wataalamu hutembelea maeneo vijijini.

# Nyati wasababisha taharuki kijijini

**Na Gurian Adolf,** KALAMBO

NYATI sita wamevamia Kijiji cha Ilimba, Wilaya ya Kalambo, mkoani Rukwa na kuzua taharuki kwa wananchi pamoja na kushindwa kuendelea na shughuli za uzalishaji wakihofia maisha yao.

Jana wakati baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi likiendelea, Diwani wa Kata ya Sunda, Peter Simuyemba, alitoa taarifa katika kikao hicho kuwa kundi hilo la nyati limevamia kijijini hapo na kuzua hofu kwa wananchi.

Alisema kuwa, wakazi wa kijiji hicho hivi sasa wamejifungia ndani ya nyumba zao wakishindwa hata kuendelea na shughuli za uzalishaji, hivyo wanaiomba halmashauri kupitia idara ya maliasili iwasaidie kuwaondoa wanyama hao.

Diwani huyo alisema kuwa kijiji kicho kimekuwa na kawaida ya kuvamiwa na tembo kila mwaka kipindi cha masika na wamekuwa wakila mazao ya wakulima na kuwasababishia hasara kubwa na njaa kwa kukosa mavuno.

Baada ya taarifa hiyo, Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Daud Sichone, aliiagiza idara ya maliasili kufika kijijini humo na kuwarudisha nyati hao katika mapori ya akiba, pia aliwataka wananchi wa vijiji hivyo kuendelea kuchukua tahadhari, ili kuepuka madhara yanayoweza kukitokeza.



Wananchi wakibomoa nyumba zao ili kupisha upanuzi wa barabara katika eneo la Mabibo, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Benki ya Malawi kuwekeza ACB mfumo wa kidigitali

**Na Enock Charles**

BENKI ya Biashara Akiba (ACB) imesema ipo mbioni kufungua ukurasa mpya wa kibiashara kwa kujenga mfumo thabiti wa utoaji huduma kidigitali, baada ya kupata mwekezaji wa kimkakati ambaye ni Benki ya Taifa ya Malawi (NBM).

Ubia huo kati ya ACB na NBM uliofikiwa hivi karibuni, unalenga kuijenga zaidi benki hiyo kwa kutanua mtandao wake wa huduma za kifedha nchini na kuhimili ushindani miongoni mwa watoa huduma.

Dora Saria, Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa ACB, alisema jana jijini Dar es Salaam, kuwa ubia huo ni wa muda mrefu na umeshaanza kuonyesha matunda kama vile kuanzishwa kwa huduma ya Akiba wakala.

"Benki imepata mwekezaji wa kimkakati, ambaye ni Benki ya Taifa ya Malawi (NBM). Tuna imani kwamba ubia huu utasaidia kupanua wigo wetu wa kibiashara ikizingatiwa NBM ni moja ya benki kubwa kwenye ukanda wetu wa nchi za kusini mwa Afrika. Ushirikiano tuliouanzisha kati yetu na NBM umeleta ari kubwa, ambayo siyo tu ya kuhakikisha huduma za benki zinapatikana nchi nzima bali zinapatikana kidigitali na kwa uhakika," alisema Saria.

Alisema mchakato wa kuibadili benki kuwa ya kidigitali unaendelea vizuri na una uhakika kuwa, utaleta unafuu na kuokoa gharama za upatikananji wa huduma.

Kwa sasa benki inatoa huduma ya Akiba Mobile, ambayo inawezesha wateja wetu kufanya malipo ya LUKU, ving'amuzi, muda wa maongezi pamoja na malipo yote ya Serikali.

Alisema benki ya Akiba siku zote imekuwa mstari wa mbele katika kufanya utafiti mbalimbali kuangalia mahitaji ya soko na wateja wake kwa ujumla, kwani inatambua umuhimu wa kutoa huduma zinazoendana na mahitaji ya soko.

Akizungumzia huduma ya Akiba Wakala ambayo imeanza kutolewa takribani wiki tatu sasa, Saria alisema tayari imeanza kutoa matokeo mazuri kwa kuwezesha wateja kupata huduma kwa urahisi zaidi popote pale walipo. "Tunaamini kwamba, kupitia huduma hii benki inakuwa mshiriki mzuri katika kuunga mkono harakati za Serikali za kuhakikisha uwapo wa huduma jumuishi za kifedha yaani kwa Watanzania wote," alisema na kuongeza:

"Tumeingia sokoni na jumla ya mawakala wapatao 200, na lengo letu ni kuendelea kuongeza mawakala wengi kadri iwezekanavyo kwa lengo la kukidhi kiu ya upatikanaji wa huduma hii nchi nzima bila ulazima wa mteja kuja kwenye matawi ya benki."

# Fursa yaja uwekezaji kwenye viwanda 20

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, ametangaza fursa za uwekezaji katika viwanda 20 vilivyokuwa vimebinafsishwa na kurejeshwa serikalini.

Prof. Mkumbo aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam kuhusu fursa za kuwekeza katika viwanda vilivyobinafsishwa na kurejeshwa serikalini.

Alisema serikali ilifanya tathmini mwaka 2017 katika viwanda 156 vilivyobinafsishwa tangu mwaka 1990 na kubaini kuwa 88 vinafanya kazi kwa kuzingatia matakwa ya mikataba husika na 68 vilikuwa havifanyi kazi kwa mujibu wa mikataba husika.

Waziri alisema serikali iko katika hatua ya kurudisha viwanda 48 kati ya 68 visivyofanya kazi kwa mujibu wa mikataba husika kwa hatua zingine za uwekezaji, ambapo hadi sasa 20 havina mgogoro wa kisheria na viko katika hatua ya uwekezaji.

Prof. Mkumbo pia alisema utaratibu wa kuwekeza katika viwanda hivyo 20 kwa kuvigawa 10 kwa wawekezaji kutoka sekta binafsi ili waviendeleze, viwanda nane vimekabidhiwa kwa Mamlaka ya Maeneo ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje EPZA kwa ajili ya wawekezaji katika maeneo hayo na viwili vitakabidhiwa mashirika ya umma ili waviendeleze kwa kuingia ubia na wawekezaji wa sekta binafsi.

Viwanda 10 vitakavyokabidhiwa kwa sekta binafsi kwa ajili ya uwekezaji ni pamoja na Kiwanda cha Kilimanjaro Paddy Hauling kilichoko Kilimanjaro, Polysacks Company Ltd kilichoko Dar es Salaam, NMC Isaka Rice Mill Company Limited kilichoko Shinyanga na Multipurpose Oil seed Processing Co.ltd (MOPROCO), kwa mujibu wa Prof. Mkumbo.

Vingine ni CDA Intergrated Concrete Industry kilichoko Dodoma, Manawa Generies Ltd kilichoko Mwanza, NMC Tabora Rice Mill kilichoko Tabora, Musoma Textikes Mills kilichoko Musoma, NMC Mzizima Maize Mill kilichoko Dar es Salaam na Pesticides Manufacturers limited - Moshi kilichoko Kilimanjaro.

Viwanda nane vinavyokabidhiwa kwa EPZA ni Mwanza Tanneries kilichoko Mwanza, TPL Shinyanga Meat Plant kilichoko Shinyanga, Mafuta Ilulu kilichoko Lindi, Nachingwea Cashewnut kilichoko Lindi, TPL Mbeya kilichoko Mbeya, Sikh Sawmill Limited kilichoko Tanga na National Steel Corporation kilichoko Dar es Salaam.

Prof. Mkumbo alisema viwanda viwili vitakavyokabidhiwa Mashirika ya Umma ni Mag'ula Mechanical MachineTolls kilichoko Morogoro kitakabidhiwa kwa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na Mbeya Ceramics Co. Ltd kitakabidhiwa kwa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

Aidha, alisema wawekezaji wenye nia na uwezo wa kuwekeza katika viwanda hivyo wawasilishe maombi yao Ofisi ya Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara ambapo zoezi la kuwapata wawekezaji litafanyika kwa uwazi na ushindani na taratibu za maombi hayo zitatolewa katika vyombo vya habari.




Mkuu wa Mauzo na Usambazaji wa Vodacom Tanzania Plc, George Lugata akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, wakati akitangaza kuungana na kampuni ya Samsung, kuzindua simu mpya aina ya Samsung A22. Kulia ni Meneja wa Samsung Tanzania, Suleiman Mohamed. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watatu kortini madai kusafirisha kilo 10 heroine

**Na Beatrice Inyasi, TUDARCo**

WATU watatu wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, wakituhumiwa kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine zenye uzito wa kilogramu 10.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, Joseph Luambano, jana Wakili wa Serikali, Ashura Mzava, alidai kuwa watuhumiwa hao walikamatwa Agosti 11, mwaka huu, katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Mwalimu Julius Nyerere.

Watuhumiwa hao ni Mohamed Kassim Yusuf (35), Sania Said Kombo (33) na Nasri Ally Khamis (33), wote wakazi Mombasa Zanzibar.

Aidha, washtakiwa hao hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Upande wa mashtaka ulidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na imeahirishwa hadi Septemba 7, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

# Vijana wapewa jukumu utatuzi migogoro Pemba

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

VIJANA kisiwani Pemba wametakiwa kushirikiana katika kuhakikisha wanatatua migogoro inayoweza kutokea ndani ya jamii.

Akizungumza na viongozi wa kwenye jamii na taasisi katika mkutano wa utatuzi wa migogoro kwa njia shirikishi, ambao ulifanyika Chake Chake, Afisa Mradi wa Dumisha Amani Pemba, Khamis Abbasi Khamis, alisema, kila mmoja anayo haki ya kudumisha amani.

Alisema vijana wana mchango mkubwa wa kuhakikisha kwamba hawasababishi migogoro, badala yake wawe ni sehemu ya kuitatua, ili jamii iwe na amani.

"Tunaona kwamba baadhi ya vijana hutumiwa kwa lengo la kusababisha migogoro na hatimae kuchafua amani, jambo ambalo kuirejesha ni gharama kubwa, hivyo tujitahidi kutatua migogoro ndani ya jamii yetu na sio kusababisha," alisema.

Aidha, alisema migogoro ni kitu kisichoepukika ndani ya jamii, hivyo ni vyema kabla ya kutatua, kwanza wajitambue na ndipo waanze kutatua, kitu ambacho kitawarahisishia katika utatuzi wa migogoro hiyo.

Kwa upande wake Afisa Habari kutoka Shirika hilo, Khelef Nassor, alieleza mkutano huo ni utekelezaji wa mradi wa Dumisha Amani, ambao utatekelezwa kwa miezi 18 kwa Zanzibar.

"Tunatoa mafunzo haya kwa makundi mbali mbali, ili kuhakikisha kwamba tunaondoa migogoro na mifarakano, ambayo mara nyingi hujitokezea baada ya kumaliza uchaguzi mkuu nchini," alisema Khelef.

Aliwataka washiriki wa mafunzo hayo waifikishe elimu hiyo katika jamii sambamba na kusaidia kutatua migogoro kwa kutumia njia sahihi, ili amani iweze kudumu.

Mshiriki, Warda Waly Mohamed, aliwataka washiriki wenzake kufuatilia chanzo cha mgogoro na ndipo waanze kusuluhisha, na kuwa hiyo itawapa wepesi katika kufikia lengo.

"Tuna tabia ya kuangalia jambo pale tunapoona tu, tunasahau kwamba kuna mzizi wake, tukiwa tutaangalia hivyo, naamini tutafanikiwa kutatua migogoro na jamii itaishi kwa amani," alisema.

Mshiriki Ali Juma, alisema ni vyema wakasimamia katika kuondoa migogoro na wasiwe ni chanzo cha kuvunja amani, hivyo washirikiane kuhakikisha vijana hawatumiliwi vibaya na watu wachache wasiopendelea mema nchi yao.

Nae mshiriki, Mohamed Abrahaman Shehe, alisema mafunzo waliyopewa ni muhimu sana na wamepata uelewa wa mambo mbalimbali ambayo yatawasaidia katika kutatua migogoro kwenye jamii.

Mkutano huo wa siku tatu wa utatuzi wa migogoro kwa njia shirikishi, uliwashirikisha maofisa wa serikali, viongozi wa jamii, wakiwamo masheha, viongozi wa mabaraza ya vijana, walimu na viongozi wa taasisi zisizo za kiserikali.

ama
ALHAMISI AGOSTI 26, 2021
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 12

Baada ya GBV kuwaathiri kiafya, kinamama waungana kuikabili



Ukurasa 14

Wajawazito mmesikia ni ruksa kuchanjwa UVIKO- 19 ila...

# Kuupuuza UVIKO-19 sasa kwaiibua CHAKUA

## •Wajitosa ndani ya vyombo vya usafiri, stendi



Katibu wa CHAKUA Kanda ya Kaskazini, Godwin Mpinga, akitoa elimu ya kujikinga na UVIKO-19 kwa abiria ndani ya basi, jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Sabato Kasika**

VITA dhidi ya UVIKO-19 imepata nguvu mpya baada ya Chama cha Kutetea Abiria (CHAKUA) kusambaza maofisa wake kuhamasisha abiria ndani ya mabasi kuchukua tahadhari. Hatua hiyo inafuatia hali ya kusuasua kujihadhari na ugonjwa huo inayoonekana kwenye maeneo na mikoa mingi nchini.

Wahamasishaji hao, wapo mikoa yote ya Bara wakiendelea kutoa elimu ndani ya daladala, mabasi makubwa na kwenye vituo vya mabasi hasa vikubwa.

Msemaji wa CHAKUA, Solomon Nkiggi, anasema, wanahimiza abiria na wananchi maeneo hayo kuvaa barakoa, kunawa mara kwa mara, kutumia vitakasa mikono, lakini pia kuepuka kula ovyo bila kunawa na kuzingatia maelekezo ya mwongozo wa afya kujikinga na corona.

"CHAKUA tuna nafasi ya kuhakikisha abiria wanakuwa salama wanapoanza safari hadi wanapofika mwisho, hivyo tunashiriki kikamilifu kutoa elimu ya kujikinga na corona," anasema Nkiggi.

Kwa mujibu wa Nkiggi, wanachukua hatua hiyo, baada ya kubaini kuwa tangu mwongozo utolewe, abiria wengi na hata makondakta na madereva hawajabadilika, hali inayoweza kuchangia kuenea kwa ugonjwa huo.

"Maelekezo ya serikali yanaagiza wasafiri kuwekewa miundombinu ya kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka kabla ya kuingia kwenye vyombo vya usafiri, lakini kuna sehemu mambo hayo hayatekelezwi," anasema.

Msemaji huyo anaongeza kuwa, wamiliki wa vyombo vya usafiri wanaelekezwa kuweka vitakasa mikono katika vyombo hivyo, kwa usalama wa afya za abiria.

Aidha, CHAKUA mbali na kutoa elimu ya kujikinga na ugonjwa huo, anasema, chama hicho kinahimiza viongozi wake na wanachama kupata chanjo ya corona kwa ajili ya usalama wa afya zao na wa abiria pia.

### OMBI KWA WIZARA

Katibu wa CHAKUA kanda ya kaskazini, Godwin Mpinga, anaiomba Wizara ya Afya, halmashauri na wadau wengine, kusambaza vifaa vya kunawia mikono kwenye vituo vya mabasi vinavyozingatia mahitaji ya wenye ulemavu.

Anasema, katika kanda hiyo, serikali imeweka huduma hizo katika stendi kuu za mabasi, ili kukinga wananchi dhidi ya corona, lakini inahitajika zaidi kuwakumbuka wenye uhitaji maalumu.

"Kwenye stendi kuu ya mabasi Arusha kuna matangi madogo ya maji na sabuni, lakini wakati maji yanaisha hayawekwi mengine kwa wakati. Lakini pia hakuna vifaa ambavyo ni rafiki kwa walemavu," anaongeza.

Anasema, kuna haja ya kuweka miundombinu ambayo ni rafiki kwa kundi hilo ambalo mara nyingi halifikiwi na huduma hizo kutokana na kukosekana miundombinu rafiki.

"Kwa mfano tangi la maji na sabuni vimewekwa juu kwenye ngazi maalum ambako mlemavu hawezi kufikia. Tunashauri miundombinu hiyo iwe rafiki kwa kundi hilo ili kila mmoja ahudumiwe," anasema.

### KUSIMAMIA MWONGOZO

Julai mwaka huu, Wizara ya Afya, ilieleza kuwa wagonjwa wa UVIKO -19 walifikia 682 na kutoa mwongozo mpya wa kudhibiti ugonjwa huo.

Takwimu hizo zilitolewa na Waziri wa Afya, Dk. Dorothy Gwajima, zilifuatiwa na maelekezo ya Katibu Mkuu, Profesa Abel Makubi, akatoa mwongozo mpya unaoelekeza namna ya kujikinga na maradhi hayo.

Mwongozo huo unaainisha kuepuka misongamano katika shughuli za kijamii, ndani ya vyombo vya usafiri, kwenye vituo vya mabasi ya mijini na mikoani.

Aidha, ndani ya daladala abiria wakae kulingana na idadi ya viti 'level seat', lakini bajaj na bodaboda madereva na wateja wao wavae barakoa na kuepuka msongamano wa abiria, kwa kuwa ugonjwa huo unaweza kusambazwa kupitia vyombo vya usafiri.

Hata hivyo, pamoja na kuwapo kwa mwongozo huo, bado hakujawa na mabadiliko kwenye baadhi ya vyombo hivyo na Dar es Salaam hali ni mbaya zaidi, kwa vile maagizo hayo yanapuuzwa kila mahali isipokuwa hospitalini, ndani ya mwendokasi na ofisi zinazosimamia na kutekeleza mwongozo huo.

### KUDHARAU UGONJWA

Mkazi wa jijini Dar es Salaam anayejitambulisha kwa jina la Shaban Bata, anasema, licha ya

INAENDELEA UK.12

AFYA

# Baada ya GBV kuwaathiri kiafya, kinamama waungana kuikabili




Mkuu wa Polisi Kituo cha Kilwa(OCS), Anna Komba, anawapa wazazi ujumbe wa kuimarisha ulinzi na malezi bora kupunguza ukatili .PICHA: MWANDISHI WETU.

**Na Mwandishi Wetu**

UKATILI wa kijinsia (GBV) unaathiri afya na wakati mwingine unaweza kusababisha vifo. Katika moja ya ripoti za Shirika la Afya Duniani (WHO) ukatili wa kijinsia ni moja ya vyanzo vya vifo vya watu wengi wenye umri wa kati uya miaka 15-44 duniani na kwamba asilimia kubwa ya vifo hivyo ni vya wanawake.

Ukatili wa kijinsia upo nchini na katika Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi mambo kama kutelekeza wanawake na watoto, kunyimwa ardhi, kubaka, kunajisi na ndoa za utotoni hata kuoza wanafunzi usiku ni jambo lililoota mizizi.

Baadhi ya kinamama wanataabika kiakili, kimwili na hata kuishi na sonona. Suala hilo linaibuka wakati wa ziara ya wanahabari kutembelea miradi ya shirika la ActionAid, wilayani Kilwa hivi karibu.

Wanawake wanasema zipo sababu nyingi lakini mojawapo ni kilimo, wakisema wakazi wa Kilwa ni wakulima wa ufuta na korosho na baadhi husafiri kwenda mbali na kuacha familia nyumbani, na huo huwa mwanzo wa mabinti kubakwa na watoto kunajisiwa .

Watuhumiwa hufanya hivyo wakiamini kuwa watoto hawana ulinzi wala mahitaji ya kutosha hivyo ni rahisi kuwarubuni.

Wanasema jambo jingine ni kukosekana maji. Vijiji vingi kama Matandu, Njinjo, Mandawa, Maguruwe, Kipindimbi, Mitole na Ngea havina maji safi na salama ya bomba au visima, hivyo kulazimisha wasichana kutafuta maji hata usiku wa manane visimani na mabondeni.

Hapo baadhi hubakwa au kudanganywa na wanaume wanaowataka kiuhusiano wakiwaeleza kuwa watakuwa wanawachotea maji na kuwapa mahitaji ya muhimu.

Hata hivyo, juhudi mbalimbali zinafanywa kuwahamasisha wanawake, watoto na mabinti kukabiliana na unyanyasaji kwa kuwafundisha ujasiri na kuripoti unyanyasaji polisi, ustawi wa jamii na kushirikiana kuwafikisha wahusika mahakamani.

Tumaini Jipya la Wanawake Kilwa (TUJIWAKI), ni jukwaa la kuhamasisha mabadiliko na kupinga ukatili wa kijinsia na kutetea haki za wanawake wilayani humo.

Asasi hiyo iliyoanzishwa mwaka 2016 kwa kushirikiana na ActionAid Kilwa, imeelimisha jamii kuhusu athari za ukatili huo na sasa wanawake wameamka wanaripoti polisi, mabaraza ya ardhi, ustawi wa jamii hadi mahakamani udhalilishaji.

Anasema Pili Kuliwa, Katibu wa TUJIWAKI Kilwa, na kuongeza kuwa wamefungua miduara (vikundi)14 kwenye vijijini mbalimbali kuhamasisha mabadiliko.

Anasema wanawake zaidi ya 2,500 wamefunzwa kuhusu ukatili wa kijinsia na kwa kutumia njia mbalimbali kama simu, mikutano ya vijiji, siku za kitaifa kama ya wanawake duniani, ya mtoto wa Afrika, UKIMWI na siku ya mtoto wa kike wamehamasisha kupinga matendo hayo na sasa kuna mabadiliko.

"Kwa kutumia ujumbe kama wa simu, redio za kijamii, maonyesho mbalimbali na mikutano vijijini tumewafikia zaidi ya watu 10,000 na kuongeza ufahamu dhidi ya ukatili huu.

"Wanawake sasa wanafahamu athari za unyanyasaji, wanaweza kusimama kujitetea na kudai haki zao licha ya kwamba bado kuna kazi," anasema Pili.

TUJIWAKI iliyoanzishwa rasmi miaka minne iliyopita, Pili anasema ina wanachama 520 katika kata 14 za wilaya ya Kilwa na kwamba wana mengi ya kujivunia ikiwa pamoja na wanawake waliotalikiwa kudai na kupata haki zao.

Pili anasema: "Kuna wanachama wetu wawili waliotalikiwa na kutimuliwa lakini kwa kutumia mafunzo na hamasa waliyopewa walifika mahakamani kudai haki na sasa wameanza maisha upya licha ya kupokonywa kila kitu na kufukuzwa. Leo wamepata tena haki zao.'"

Anasema hawajaishia hapo wamekwamishwa ndoa za watoto watano na kuwarejesha shuleni na sasa wanaendelea na masomo.

Pili anaeleza kuwa kuna mengi ya kujivunia ikiwa ni pamoja na kufanikisha kuwarudishia huduma watoto wanne waliokuwa wametelekezwa na baba zao, lakini sasa wamewapokea na wanawahudumia.

Anasema kazi hiyo inafanywa kwa kushirikiana na ofisi ya ustawi wa jamii pamoja na polisi.

Anaeleza kuwa TUJIWAKI imeamua kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ya kuendeleza na kusaidia maendeleo ya wanawake na sasa wanajenga ofisi ya kutoa huduma itakayogharimu takriban Shilingi milioni 83 msaada wa ActionAid Kilwa.

Takwimu kutoka wilayani Kilwa zinaonyesha kuwa mwaka 2019 wanafunzi 160 walipata ujauzito mkoani Lindi, wakati mwaka 2020, waliopata ujauzito walikuwa 75.

Zinaongeza kuwa wilayani Kilwa kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu mabinti 40 walipewa mimba.

Anna Tembo OCS wa Polisi Wilaya ya Kilwa, anapozungumza na wanahabari anasema, unyanyasaji wa kijinsia ni tatizo kubwa katika wilaya hiyo, akihusisha shida hiyo na malezi duni na wazazi pamoja na walezi kutojali watoto.

Anataja mafunzo na ngoma za kuwafundisha mabinti masuala ya watu wazima, kuishi na wenza wakati walitakiwa shuleni, kuwa yote hayo yanachangia mimba utotoni na utoro shuleni.

Anasema katika kutibu suala hilo Polisi Wilaya ya Kilwa inafanya mafunzo shuleni kuwahamasisha watoto hasa mabinti kuamka na kupinga ukatili dhidi yao na kufikisha ripoti polisi, kwa walimu, wazazi na ustawi wa jamii wanaponyanyaswa.

"Tumewafundisha wanafunzi wa primari na sekondari za Kilwa Masoko. Tumefika sekondari za Mnazi na Kilwa Day, Shule ya Msingi Kwa Sultan na Sekondari ya Kilwa Masoko na watoto takribani 1,079 wamenufaika.

## Kuupuuza UVIKO-19 sasa kwaaibua CHAKUA

**INATOKA UK.11**

maelekezo ya serikali ya kujikinga na ugonjwa huo ndani ya vyombo vya usafiri, baadhi ya abiria, makondakta na madereva ni wabishi.

"Tunaelekezwa kwamba, kila abiria anayeingia kwenye chombo cha usafiri wa umma lazima avae barakoa, wengine hawafanyi hivyo, wanadai kwamba hakuna ugonjwa, corona ni ugonjwa wa wazee , matajiri au kama umeandikiwa kufa utakufa tu..." anasema Bata.

Anasema, daladala zinatakiwa kupakiza abiria 'level seat' na kuvaa barakoa, na kwamba hilo nalo halizingatiwi, badala yake abiria wenyewe, makondakta na madereva hawachukui tahadhari na msongamano uko pale pale.

"Binafsi nimefuatilia sana mwongozo huo, unaelekeza pia bodaboda wasibebe mishikaki na kuvaa barakoa lakini hilo nalo halifanyiki...," anasema.

Anaongeza kuwa, stendi kunatakiwa kuwe na ujumbe wa kuelimisha wasafiri mara kwa mara kupitia vipaza sauti na wanapokuwa safarini, madereva na wahudumu wa vyombo vya usafiri wahakikishe ujumbe wa kuelimisha unatolewa katika chombo mara kwa mara, yote hayajaonekana.

"Ukienda kwenye vituo vya daladala utakutana na msongamano nje na ndani ya mabasi hayo na muziki unaosikika ni bongofleva na singeli bila ujumbe wa kuhamasisha kuchukua hadhari.

AFYA

## BINGWA AONYA

# Mila potofu zisiwe kikwazo kwa maziwa ya kwanza

## •Yasitupwe ni chanjo, tiba kwa watoto

**Na Maulid Mmbaga**

MAZIWA ya mama kwa mtoto mchanga mara tu anapozaliwa yana umuhimu wa kipekee kwa sababu ya virutubisho vilivyo ndani yake ambavyo humpa mtoto kinga ya magonjwa na kuimarisha ufahamu au utimilifu wa akili.

Lakini licha ya umuhimu huo imani potofu kuwa maziwa ya kwanza yenye rangi ya njano si salama kwa mtoto, inaendelea kukwamisha juhudi za unyonyeshaji, pengine si Tanzania pekee bali Afrika na Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Maziwa hayo ya kwanza au 'colostrums', ndiyo ya muhimu zaidi kuliko mengine yoyote atakayopewa, ni kama chanjo ya kwanza kwa binadamu na yana virutubisho vingi na pia kinga ambazo zinamuepusha mtoto na maradhi mbalimbali, anasema Dk.Peter Daudi, kutoka Hospitali na Kituo cha Utafiti wa Magonjwa ya Kuambukiza cha Kibong'oto.

Mtaalamu huyo wa watoto, anasema utafiti unaonyesha kuwa asilimia kubwa ya kinamama maziwa yao yanatosha kabisa katika kumnyonyesha mtoto kwa miezi sita.

Wakati anayasema hayo, baadhi ya jamii huwahimiza wazazi kukamulia chini maziwa hayo kwa maelezo kuwa hayafai kwa mtoto huku wengine wakiamini kuwa yanamuumiza tumbo.

Mathalani, jamii za kanda ya ziwa zinaelekeza mama anapojifungua kabla ya kumnyonyesha mtoto, kukamulia maziwa hayo ukutani hadi yanapokuwa meupe, bila kujua kuwa wanaharibu kitu muhimu kwa maisha ya binadamu.

Essong Jerry, mwanahabari kutoka Cameroon, anayeishi Tanzania anaeleza kuwa hata katika taifa lake, kuna mila potofu zinazowataka wanawake kuyakamulia chini na kuufanya mwiko kumnyonyesha mtoto maziwa ya njano.

Dokta Daudi, anasema kuhamasisha unyonyeshaji kutamaliza tatizo hilo baada ya kinamama kuelimishwa umuhimu wa maziwa hayo kazi inayotakiwa kufanyika kliniki na hata vijijini.

Anaendelea kusema kuwa, tatizo lililopo ni kuwa kinamama wengi hufikiria hawana maziwa ya kutosha kwasababu utengenezaji wa maziwa pia unahusisha saikolojia ya mama mwenyewe, kama ana mawazo mengi, msongo na kuchoka vyote huchangia kuyapunguza.



Maziwa ya mwanzo yenye rangi ya njano ni tiba, chanjo na kinga ya kudumu. Mama amnyonyeshe mtoto asiyatupe. **PICHA:MTANDAO.**

### MTOTO ASIPEWE MAJI

Dokta Daudi, anafafanua kuwa maziwa ya kwanza ni muhimu na yana virutubisho vyote muhimu kina mama wasiyatupe. Yana maji hivyo mtoto anayenyonya ndani ya miezi sita hahisi kiu na hahitaji maji.

Akifafanua sababu za mtoto kulia na kuibua hofu kwa mzazi, anasema kunatokana na sababu mbalimbali, lakini kunyonyesha kunaweza kumbembeleza na kama mama atafuata maelekezo yote maziwa yatatosha na atashiba vizuri, lakini pia ni vizuri kujua mambo mengine yanayosababisha mtoto kulia.

Anawashauri kinamama wanaohofu kuwa wakianza kazi baada ya miezi mitatu watoto hawatashiba na kuanza kuwapa watoto maziwa ya kopo, ya ng'ombe au uji mwepesi kuwa wanakosea.

"Kabla ya kwenda kazini unaweza kukamua na kuyatunza kwenye jokofu na kuyagandisha, yanaweza kukaa kwa siku nyingi bila kuharibika na kufanya mtoto wako aendelee kupata maziwa yako, hiyo inamsaidia mtoto asipate vyakula vingine kabla ya miezi sita." Anasema Daudi.

Anakumbusha kuwa mtoto anapaswa kunyonya ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa kwa kufuata masharti ya kiafya yanayohusu unyonyeshaji, na anaweza kunyonya mpaka angalau miaka miwili, akilishwa vyakula vingine baada ya kunyonya maziwa ya mama pekee kwa miezi sita.

"Maziwa ya mama ni muhimu sana kwa mtoto kwasababu yanajenga kinga imara ya mtoto, yanamfanya awe na makuzi bora ya ubongo, hivyo mtoto anapoyakosa lazima atapata shida kimakuzi pia atakuwa katika hatari ya kupata magonjwa mara kwa mara."

### KINACHOKWAMISHA MAZIWA

Anataja baadhi ya sababu zinazomfanya mama asitoe maziwa ya kutosha kuwa ni pamoja na matatizo ya vichocheo au 'hormones', mama anapojifungua kama atakuwa na matatizo mfano kisukari yanaweza kukwamisha maziwa.

Daktari anataja matumizi ya dawa za kupanga uzazi zenye vichocheo'

akisema, kama mama aliyejifungua ataanza kuzitumia kabla mtoto kufikisha miezi minne, inaweza kusababisha maziwa kupungua.

Wakati mwingine upungufu wa maziwa unatokana na matumizi ya baadhi ya dawa za kusaidia kuharakisha kujifungua kama epidural anaesthetic' zinaweza kupunguza maziwa, anasema Dk. Daudi.

"Kumuongezea mtoto maziwa ya kopo pale baadhi ya kinamama wanapojifungua siku ya kwanza kwa vile maziwa hayatoki, iwapo ataanza kupewa maziwa kwenye hatua za mwanzo kabisa itasababisha matiti yasitengeneze maziwa kwa kiwango cha kutosha," anaonya na kukumbusha kuwa maziwa yatatoka kwa wingi kama mzazi atamnyonyesha mtoto mara kwa mara kwani kufanya hivyo kunachochea utengenezaji wa maziwa.

Anataja kutomyonyesha mtoto usiku kuwa ni sababu nyingine ya kupungua maziwa.

"Ni kawaida kwa mama anayenyonyesha kutopenda kumyonyesha mtoto usiku ili alale, tabia hii ikiendelea inapunguza kiwango cha maziwa kinachotengenezwa kwasababu usiku vichocheo vinavyosisimua utengenezwaji wa maziwa vinafanyakazi zaidi, hivyo kuongeza uzalishaji na kama hanyonyeshi usiku, mwili utahisi hayahitajiki na kiwango kitashuka," anabainisha.

Dokta Daudi anataja sababu ya mtoto kutonyonya ipasavyo inaweza kuyapunguza kwani anatakiwa kuvuta maziwa kikamilifu kwenye chuchu na akishindwa inaweza kupunguza utokaji.

Kukosa lishe bora na virutubisho mama anapokuwa mjamzito na anapojifungua, kuimarisha afya yake na ya mtoto pamoja na kutengeneza maziwa ya kutosha na kuepuka mtoto kuwa na utapia mlo ni sababu nyingine.

Msongo wa mawazo pia unahusika kwa vile mama anayenyonyesha anapokuwa na hali hiyo kutokana na sababu mbalimbali inaweza kuchangia kukausha maziwa.

Kwa mujibu wa Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), mama anayenyonyesha anatakiwa kuwa na lishe bora yenye aina zote za virutubisho kutokana na mahitaji makubwa kwa ajili ya afya yake na kutengeneza maziwa ya mtoto na kushauriwa kula milo kamili zaidi ya mitatu kwa siku na vyakula vingine kati ya mlo na mlo.

TFNC inaeleza umuhimu wa ulaji unaofaa kwa mama anayenyonyesha kwa sababu humpatia afya bora na virutubisho vya kutosha kukidhi ongezeko la mahitaji yake na ya mtoto anayenyonya na kuuwezesha mwili kutengeneza na kutoa maziwa ya kutosha wakati wote.

Lishe bora ni kinga na tiba ya kuzuia upungufu wa damu kwa mama na mtoto, aidha huongeza akiba ya madini chuma ambayo hutumika kwa mama na kwa mtoto kuzalisha damu.

### MAMBO YA KUZINGATIA


TFNC inamshauri mama kula milo kamili zaidi ya mitatu kwa siku yenye mchanganyiko angalau chakula kimoja kutoka katika kila kundi la chakula na kula chakula kingi na cha kutosha katika kila mlo, kupata asusa (vyakula vingine) kati ya mlo mmoja na mwingine, kumeza vidonge vya kuongeza damu (FEFO) kwa kipindi cha miezi mitatu baada ya kujifungua, kutumia vyakula vilivyoongezwa virutubisho.

Hivyo ni pamoja na unga wa ngano, wa mahindi, mafuta ya kupikia na kutumia chumvi yenye madini joto, pia kuongeza ulaji wa nyama, kuku, samaki. Kutumia mayai, maziwa na vyakula vyenye madini chuma kuongeza damu mwilini.

Matunda ya aina mbalimbali na mbogamboga kwa wingi, kunywa maji ya kutosha kila siku angalau lita 1.5 kwa siku ni muhimu pia.

AFYA

# Wajawazito mmesikia ni ruksa kuchanjwa UVIKO- 19 ila...



Dk. Matilda Ngarina

**Na Christina Mwakangale**

TANGU kuwapo kwa maambukizi ya virusi vya corona duniani hadi jitihada za kupatikana chanjo zilipofanikiwa hivi karibuni, suala la wajawazito na wanaonyonyesha kupewa chanjo linaendelea kuhitaji ufafanuzi na taarifa zaidi.

Makundi ambayo yalipewa kipaumbele kuchanjwa ni pamoja na wataalamu wa afya, wazee, wenye magonjwa yasiyoambukiza na watu walio katika huduma au kazi zinazowakutanisha na mamia ya watu.

Hata hivyo, suala la wajawazito na wanaonyonyesha kupata chanjo hiyo halikutajwa kwa kiwango kikubwa hasa kwa baadhi ya nchi, hivyo, kuibua hisia kuwa huenda wanaweza kuathirika iwapo wangechanjwa.

Kufuatia hatua hiyo, Chama cha Madaktari wa Magonjwa ya Wanawake na na Uzazi Tanzania (AGOTA), hivi karibuni kimetoa ufafanuzi kuhusu mustakali wa wajawazito na wanaonyonyesha kuchanjwa, na kushauri wachanje.

Mabingwa 10 wanachama wa Chama cha Madaktari wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi katika andiko hilo wanaeleza kuwa kundi hilo nalo linastahili kupata chanjo ya corona, lakini kwa kuchukua tahadhari kwa kujua hali ya afya zao.

Bingwa wa Magonjwa ya Wanawake na Uzazi kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Matilda Ngarina, mmoja wa walioshiriki kuandaa andiko hilo, anasema sababu ya kutoa maelezo kuhusu wajawazito na kinamama wanaonyonyesha na chanjo hiyo kunatokana na kupokea maswali ambayo watu wameomba kupatiwa ufafanuzi.

Ngarina ambaye pia ni Rais (AGOTA), anasema kutokana na hilo wataalamu hao walikusanya taarifa za takwimu kutoka sehemu tofauti na kuja na maelezo kuwa kundi hilo linahitaji chanjo pia.

AGOTA inaeleza kuwa wajawazito wamo katika hatari ya kupata maambukizo ikilinganishwa na wengine.

Aidha, wapo katika hatari ya kujifungua mapema kabla ya wakati au kutimiza iwapo watapata COVID-19, hivyo wanahitaji kukingwa .

Inaendelea kubainisha kwamba wajawazito wanatakiwa kusubiri siku 14 iwapo wamepatiwa chanjo nyingine zinazohusiana na ujauzito, kabla ya kuchanjwa chanjo ya corona.

Pia baada ya chanjo hiyo ya corona inatakiwa kukaa siku 28 kabla ya kupatiwa chanjo nyingine ambayo inatolewa kwa wajawazito, isipokuwa kama kuna dharura kwa magonjwa kama homa ya ini itokanayo na kirusi cha Hepatitis B.

**ATHARI BAADA YA CHANJO**

Kuhusu athari baada ya chanjo AGOTA inasema iwapo umechanjwa chanjo dhidi ya corona kama ilivyo kwa nyingine hususan kwa chanjo yenye dozi mbili, wajawazito hawajaripoti athari zozote, isipokuwa kero ndogo ikiwamo homa, ambazo hupunguzwa na dawa za kutuliza maumivu kama paracetamol na panadol.

Pia baadhi hupata athari kutokana na mzio au aleji walionao baada ya kuchanjwa, na kwamba watoa huduma za afya wanatakiwa wawaulize kabla ya kuwachanja kama wana historia ya kupata madhara .

**WANAONYONYESHA**

Wakati wa kunyonyesha, AGOTA inaeleza kuwa hakuna utafiti unaoonyesha kuna athari kwa walio kwenye kundi hilo, na kwamba kinamama hao ambao hupatiwa chanjo ya corona wana kinga maalumu kupitia maziwa ambayo huwalinda watoto wao.

**WAJAWAZITO WATARAJIWA**

Kwa upande wa wanawake wanaotarajia kubeba ujauzito, AGOTA inasema kupitia utafiti uliofanyika katika nchi kadhaa hakuna taarifa rasmi zilizoonyesha madhara kwa walio katika kundi hilo iwe ni wanaume au wanawake.

**UFAFANUZI ZAIDI**

Jopo la wataalam wa afya wa mashirika ya Kimarekani hapa nchini, nalo pia lilitaja makundi ambayo hawastahili kuchanjwa UVIKO-19, lakini likaeleza kuwa wajawazito wanachanjwa lakini kwa kuangalia masuala muhimu ya kiafya. Makundi hayo ni watoto wenye umri chini ya miaka 18. Pia ni mtu anayejisikia kuumwa mfano homa siku anayotakiwa kichanjwa na wenye nzio (aleji).

Kwa upande wa wajawazito ambao wana ugonjwa wa kifua kikuu (TB) na upungufu wa damu wanatakiwa kupata ushauri wa madaktari wao kwanza kabla ya kujichanja.

> “Wenye magonjwa ya muda mrefu kama kisukari, saratani, UKIMWI na shinikizo la damu wanatakiwa kuchanja lakini kubwa ni kutoa taarifa sahihi kwa mhudumu wa afya kabla ya kuchanja ili aweze kushauri vyema,”

Daktari wa Huduma za Matibabu kwa Raia wa Marekani wanaokuja nchini kwa ajili ya kujitolea, Dk. Arkan Ibwe, anasema kwa wenye umri huo sababu ni kuwa hadi sasa hakuna utafiti wa kuthibitisha chanjo inayofaa kwao.

Anasema kwa wanaoumwa homa siku ya kuamkia kuchanjwa wanapaswa kusubiri mpaka wapone ndipo wachanje, huku wenye aleji wanatakiwa kujulikana aina ya aleji zinazowasumbua ili kuangalia chanjo itakayoendana nao ili kuepusha madhara.

Katika maelezo yake daktari wa Elimu na Afya ya Jamii na Huduma za Uzazi wa Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID), Dk.Emmanuel Tluway,anasema hakuna kinachozuia wajawazito kupewa chanjo.

“Lakini kutokana na hali zao wanashauriwa kupata ushauri kwa madaktari wao au wataalamu wa afya kabla ya kufanya uamuzi.”

Anaongeza: “Kutokana na mabadiliko ya mwili kwasababu za ujauzito wako katika uwezekano mkubwa wa kuambukizwa UVIKO-19 ni muhimu kuangalia faida na hasara kwanza. Kama faida ni kubwa basi wachanje kwa ushauri wa wataalam wa afya, hadi sasa hakuna utafiti unaozuia wasichanje na haijaelezwa kama utafiti wa chanjo uliwahusisha wajawazito,hivyo hatuna majibu ya kisayansi kwa asilimia 100,ila wanashauriwa wachanje.”

Alisema kwa wenye ugonjwa wa kifua kikuu wanapaswa kuwasiliana na madaktari wao kabla ya kufanya uamuzi, kwa kuwa wagonjwa hao huwa katika hatua tofauti.

“Wenye magonjwa ya muda mrefu kama kisukari, saratani, UKIMWI na Shinikizo la Damu wanatakiwa kuchanja lakini kubwa ni kutoa taarifa sahihi kwa mhudumu wa afya kabla ya kuchanja ili aweze kushauri vyema,”alisema Dk.Ibwe.

Kuhusu kazi ya chanjo mwilini,Dk. Tluway alisema inasisimua mwili, kuuwezesha kuamka na kupambana kwa haraka na UVIKO-19, inaimarisha kinga kwenye chembe hai (seli) nyeupe zinazohusika na kupambana na kuangamiza maradhi na kuyazuia yasiingie mwilini.

Hadi sasa Watanzania takribani 261,000 walikuwa wamepata chanjo kutoka mikoa tofauti nchini, kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Afya.





# UVCCM yazungumzia ziara za Rais Samia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), umesema ziara mbalimbali za Rais Samia Suluhu Hassan nje ya nchi ikiwamo kuhudhuria kuapishwa kwa Rais wa Zambia, Hakainde Hichilema, zinalenga kuendeleza uhusiano na nchi hizo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Katibu Mkuu wa UVCCM, Kenani Kihongosi, alisema ziara hizo ni matokeo ya uhusiano mzuri wa kidiplomasia ulioasisiwa na waasisi wa taifa na kuwataka wote wanaoweka propaganda katika suala hilo watambue kuwa taifa limejengwa katika misingi ya uhusiano na umoja.

Alimpongeza Rais Samia kwa kuendeleza uhusiano huo hususan kwa kuzingatia kuwa Tanzania imeshiriki harakati za ukombozi kwa nchi nyingi barani Afrika.

Akizungumzia kuhusu ulipaji kodi, aliwaomba wananchi kuiamini serikali yao na kuendelea kulipa kodi kwa kuwa kila senti inaenda kugusa maisha yao.

Alisema kuwa wiki iliyopita Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alibainisha Sh. bilioni 48 zimekusanywa na kugawanywa katika mambo mbalimbali ikiwamo ujenzi wa vituo 150 vya afya.

"Tunaipongeza serikali kwa kuwa fedha hizo zitaenda kurekebisha barabara na kila jimbo lilishapewa zaidi ya Sh. milioni 500, uchumi utaenda kuimarika katika maeneo ya vijijini na pato litaongezeka," alisema.

"Tunaiomba serikali fedha hizi ziende katika kazi ile ambayo imekusudiwa, walengwa husika waende wakaguswe na mambo haya yaweze kwenda vizuri."

Kuhusu wanaoitukana serikali katika mitandao, Kihongosi alisema;

"nitoe wito nidhamu ni mali na nidhamu ni uadilifu, kijana utapimwa unapokosa nidhamu kwa mzazi wako na kiongozi wako maana yake huna tofauti na msaliti lazima tuwe wazalendo tushirikiane na viongozi wetu."

Alisema hivi karibuni UVCCM itakuja na programu ya kuandaa makongamano ya fursa pamoja na dira ya jinsi gani ya kutumia vipaji ili kuondokana na tatizo la ajira.



Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima (katikati), akisindikizwa na askari wa Bunge, wakati akiingia kwenye viwanja vya bungeni, jijini Dodoma jana, kwa ajili ya kuendelea na mahojiano na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Bashe ataka sekta binafsi kuchangamkia uwekezaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ameitaka sekta binafsi kuchangamkia fursa za uwekezaji wa kutumia teknolojia ya kisasa ya unyunyiziaji dawa kwenye mazao kwa kutumia ndege maalum isiyokuwa na rubani 'Drone' ili kurahisisha utendaji kazi.

Aliyasema hayo jana jijini hapa katika ziara maalum ya kikazi ya kushuhudia teknolojia hiyo inavyofanya kazi kwenye viwanja vya wakulima Nanenane.

Bashe alisema teknolojia ya unyunyiziaji dawa kupitia ndege hiyo ina manufaa makubwa kwa sababu watalazimika kutumia muda mchache kufanya kazi eneo kubwa tofauti wangefanya zoezi hilo kupitia mikono.

"Sekta ya kilimo mnapaswa kuchangamkia fursa hii kwa sababu ina umuhimu mkubwa kuwa nayo katika utendaji kazi zenu," alisema Bashe.

Alitoa wito kwa wataalamu wanaoendesha teknolojia hiyo kuangalia jinsi watakavyowafikia wakulima wote nchini na hata waliopo vijijini.

Alisema vijijini kuna wakulima wengi na kwamba ni vyema wakaona namna ya kuipeleka teknolojia hiyo katika maeneo ya pembezoni.

"Hii teknolojia inapaswa kufika kila eneo ili wakulima wanufaike hivyo mnapaswa kuona namna ya kuifikisha vijijini ambako kuna wakulima wengi," alisema Bashe.

Alisema wanahitaji kuona wakulima wote wananufaika na teknolojia hiyo ili kufanya kilimo chenye tija.

Kwa upande wake, Mhandisi Elibari Nsenuka, ambaye ni mtaalamu wa teknolojia hiyo, alisema miongoni mwa kero wanazokabiliana nazo ni pamoja na kukosa vibali vya kurusha kifaa hicho kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TAA).

Nsenuka ambaye ni mtaalamu kutoka kampuni ya Gegro, alisema tatizo hilo linachangia wao kurudi nyuma na kuomba wizara hiyo iwasaidie kuzifanyia kazi.

Alisema lengo lao ni kuona wanafanikisha teknolojia hiyo kila maeneo ili kuisadia serikali katika sekta ya kilimo.

# Kamati zatakiwa kusimamia maadili ya mahakimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI za maadili za mahakama za mikoa na wilaya zimetakiwa kusimamia maadili ya mahakimu ili kuhakikisha wanatenda haki katika utendaji kazi.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Dodoma, Mustapher Siyani, alisema hayo alipokuwa akifungua semina kwa ajili ya kuwajengea uwezo maofisa wa kamati za maadili mikoa na wilaya.

Alisema kamati hizo ni jicho la mahakama katika kusimamia maadili ya watumishi wa umma ili kuufanya mhimili huo uzidi kuheshimika.

"Ninafahamu umuhimu wa kamati hizi za maadili, kamati hizi ni jicho la mahakama katika kusimamia na kuendeleza maadili ya utumishi wa mahakama ili kuufanya mhimili huo uwe wenye kuvutia na kutukuka," alisema.

Hata hivyo, alisema kumekuwapo na tatizo wananchi kuwa na uelewa mdogo kuhusu kazi na shughuli zinazofanywa na kamati hizo, ametaka elimu itolewe ili jamii iweze kujua.

"Uzoefu tuliupata licha ya kamati kuwapo, lakini malalamiko yamekuwa ni machache ila tumegundua ni uelewa mdogo katika kujua kama kuna tume, naomba iendelee kutoa elimu kwa njia mbalimbali ili kuwawezesha wananchi kufahamu uwapo wa kamati hizi," alisema.

"Hali halisi inaonyesha kwamba mahakimu ni vijana jambo linalolazimika kujitafutia mali, naomba tume na mahakama ziendelee kutoa mafunzo kwa maofisa wa mahakama na kamati zitumie fursa chache ili kujiepusha na ukiukwaji huo na wawe watumishi waadilifu," alisema.

Jaji Mfawidhi Siyani alisema, kamati zina wajibu wa kuzishauri tume ya utumishi wa mahakama kuhusu uzingatiaji wa maadili kwa maofisa wa mahakama pamoja na uzingatiaji wa utoaji wa huduma bora na nafuu.

"Mada zitakazotolewa ni Muundo wa Tume ya Mahakama ni matumaini yangu mtajadili suala la utawala bora na mtapokea mafunzo hayo kwa umakini mkubwa lengo muwe na ufahamu mkubwa," alisema.

Alisema endapo kamati za maadili zitafanya kazi vizuri maadili ya mahakimu yataboreka na kuwawezesha wananchi kupata haki.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya, alisema wataendelea kutekeleza na kusimamia wale wanaoitwa katika kamati hizo kuhakikisha wanatendewa haki na tuhuma zinakuwa za msingi.

"Changamoto kwa wananchi kuwa na uelewa mdogo juu ya kamati hizo jinsi zinavyofanya kazi hivyo mimi kama mwenyekiti nimejiwekea utaratibu wa kukutana na wananchi na kuwaelimisha juu ya hizi kama na jinsi gani wanaweza kuwasilisha malalamiko," alisema Msuya.



# Shehena dawa, vifaa tiba bandia yanaswa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SHEHENA ya dawa na vifaa tiba zenye thamani ya Sh. milioni 7.7 zilizokwisha muda wake, mihuri na nembo mbalimbali ambazo zinatumika kubadilisha muda wa matumizi wa dawa hizo ili zionekane mpya, zimekamatwa jijini Mbeya katika nyumba ya mtu mmoja eneo la Igawilo.

Mzigo huo ulikamatwa jana baada ya kufanya upekuzi uliyofanywa na Mamlaka ya Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi (TMDA), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, ikiongozwa na Kaimu Meneja wake, Anitha Mshighati, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi.

Mshighati alisema walipata taarifa kutoka kwa wasamaria wema juu ya kuwapo kwa mtu huyo ambaye amepaki shehena ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika nyumba yake huku akiendelea kuuza licha ya muda wake kwisha huku akitumia mihuri na vifaa vingine kubadilisha ili zionekane hazijaisha muda wake.

"TMDA tulipata taarifa uwepo wa dawa ambazo zimekwisha muda wake katika nyumba ya mkazi mmoja wa Igawilo, jijini Mbeya, zikiwamo dawa za serikali zimeonekana zikibadilishwa muda wa matumizi zionekane bado ni mpya. Tumekuta lebo na mihuri mbalimbali ili kupotosha watu kwamba bado ni mpya," alisema Mshighati.

Alibainisha kuwa dawa na vifaa tiba walivyovikamata kuwa ni antibayotiki, sindano na nyuzi za kushonea, malaria na asidi ambazo ni za serikali zikiwa zimefutwa lebo.

"Dawa zote zimekutwa katika makazi ya mtu zikiwa zimewekwa katika hali isiyofaa bila mpangilio wowote kinyume cha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura ya 219 ya mwaka 2013 kwa sababu vitu vilivyokutwa ni mali ya serikali. Tumeziorodhesha dawa zote na zimechukuliwa. Mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa ajili ya utaratibu mwingine," alisema Mshighati.

Kuhusu adhabu dhidi ya mtuhumiwa huyo, alisema mahakama ndiyo itakayoamua baada ya kuthibitisha pasipokuwa na shaka kwa sababu ni jambo la kisheria kwa sababu sheria itakayotumika ni ya dawa na vifaa tiba pamoja na ya jinai.

Akizungumzia uuzwaji na uingizwaji wa dawa zilizokwisha muda, alisema wanaendelea kufanya oparesheni maalum katika mikoa ya Songwe na Mbeya na kwamba wanashirikiana na wananchi kupata taarifa ya sehemu zinazouzwa.

Alisema wanaendelea kudhibiti mipaka ya Tunduma na Kasumulu ili dawa za magendo na zilizokwisha muda zisiingizwe nchini huku wakiendelea kutoa elimu kwa wananchi kuepukana na athari za kiafya.

Kaimu Mwenyekiti wa Mtaa wa Mwanyanje, Nessy Shitambala, alieleza kusikitishwa na tukio na mwananchi wake kukutwa na shehena ya dawa nyumbani kwake mali ya serikali ambayo zimekwisha muda wake.

Alisema mtuhumiwa huyo amekuwa akiwauzia dawa huku wakiamini huduma anayowapatia ni ya uhakika kumbe anahatarisha afya za wananchi.

Kutokana na hali hiyo, alimshauri mtuhumiwa huyo kuachana na biashara hiyo ya kuuza dawa zilizopita muda wake na ujanja anaoufanya kubadilisha lebo za muda wa matumizi ili zionekane muda haujaisha kwa kuwa amepoteza imani kwa wananchi.



Kaimu Meneja wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Anitha Mshighati, akionyesha mihuri iliyokuwa inatumika kubadilisha tarehe ya matumizi ya dawa zilizokwisha muda wake, baada ya kufanya upekuzi kwenye nyumba ya mkazi mmoja wa Igawilo ambaye alikutwa na shehena ya dawa zilizokwisha muda wake, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Miche milioni 1.6 kuzalishwa kutunza mazingira na uzalishaji wa matunda

**Na Grace Mwakalinga**, TUKUYU

WILAYA ya Rungwe mkoani Mbeya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wamepanga kuzalisha zaidi ya miche milioni 1.6 ya mbao, matunda na kivuli ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kuhifadhi mazingira.

Ofisa Maliasili wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, Castor Makeula, alisema hayo juzi wakati wa uoteshaji wa miche ya kitalu kilichoko Kata ya Bulyaga mjini hapa.

Makeula alisema miche hiyo itagawiwa bure kwa wananchi kwenye sekta binafsi na umma kwa lengo la kuwawezesha wananchi kujikwamua kiuchumi kupitia biashara ya mbao na matunda.

"Tumeamua kuzalisha miche milioni 1.6 ya aina mbalimbali kama vile matunda, mbao na kivuli ikiwa ni hatua ya kuhifadhi vyanzo vya maji, kilimo na kukuza biashara ili kukuza uchumi wa wakazi wa Rungwe sambamba na utunzaji wa mazingira," alisema Makeula.

Kwa mujibu wa Makeula, kwa sasa wanaendelea kuzalisha miche hiyo na kwamba ifikapo Januari, mwakani, wananchi wataanza kugawiwa kwa kushirikiana na maofisa ugani kutoka kila kata ya wilaya hiyo.

Baadhi ya wananchi walisema ni utaratibu mzuri ulianzishwa na wilaya kuwagawia miche ili kuendeleza jitihada za kuhifadhi mazingira na kwamba wataendelea kuitunza kwa manufaa ya kizazi cha sasa na baadaye.

Mmoja wa wananchi hao, Mary Mwangupili, kutoka kijiji cha Ilolo, alisema ni mara kadhaa amekuwa akipewa miche ya matunda na mbao na viongozi wa wilaya hiyo na kwamba ameanza kunufaika kwa kuuza maparachichi na kujiingiza kipato.

Aliishukuru serikali na kuishauri kuongeza jitihada kutunza chanzo cha maji cha mto Kilasi ili kiendelee kutoa maji katika kipindi chote cha mwaka sambamba na kupanda miti.

# Madereva bajaji, bodaboda waonywa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Mbeya, limewataka madereva wote wa vyombo vya moto mkoani hapa kuhakikisha wanafanya kazi hiyo kwa kuzingatia sheria ikiwamo kuwa na leseni ya udereva.

Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Mkoa wa Mbeya, Meloe Busema, alisema hayo juzi alipokuwa anazungumza na waendesha pikipiki za abiria, maarufu kwa jina la bodaboda na waendesha bajaji.

Alisema madereva wengi wa vyombo hivyo wamekuwa wakisababisha ajali kutokana na kutozijua sheria za usalama barabarani, hivyo akawataka kwenda shuleni kupata mafunzo ya udereva.

Busema alisema jeshi hilo kwa kushirikiana na moja ya vyuo vya udereva jijini Mbeya, wameandaa mafunzo kwa madereva hao ili kuhakikisha wanazifahamu sheria na kuzizingatia wakati wa kuendesha vyombo hivyo ili kupunguza ajali.

"Tumeamua kuanzisha mafunzo haya ili kuwarahisishia madereva hawa kuyapata na kupata leseni, baada ya mafunzo haya hatutegemei kumuona dereva anayeendesha vyombo hivi akiwa hana leseni ya udereva," alisema Buzema.

Mbeya, alisema ni miongoni mwa mikoa yenye vyombo vingi vya moto, hivyo mafunzo hayo ya udereva ni muhimu na hivyo akawataka hata madereva ambao tayari wana mafunzo kuhudhuria ili kukumbushwa baadhi ya misingi.

Alisema wataendelea kufanya operesheni za kukagua vyombo vya moto na madereva ili kuhakikisha vinafanya kazi kwa kufuata sheria na kupunguza ajali za barabarani.

Mkuu huyo aliwataka viongozi wa bodaboda na bajaji kuwahamasisha wanachama wao kuhudhuria mafunzo hayo ili wafanye kazi kwa kufuata sheria na kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima.

**"Tumeamua kuanzisha mafunzo haya ili kuwarahisishia madereva hawa kuyapata na kupata leseni, baada ya mafunzo haya hatutegemei kumuona dereva anayeendesha vyombo hivi akiwa hana leseni ya udereva," alisema Buzema.**



# Masoud ataka elimu ya sensa ifike kwa usahihi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud, amesema ni vyema kwa watendaji wa sensa kufanya jitihada za kuwafikia viongozi wa kisiasa na vyama vyao ili kufikishia kwa usahihi wananchi ujumbe wa elimu ya sensa ya watu na makazi.

Aliyasema hayo jana ofisini kwake Migombani, alipokutana na kufanya mazungumzo na Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi, Balozi Mohammed Hamza pamoja na watendaji wa sensa ofisi ya Zanzibar.

Alisema kufanya hivyo kutasaidia wananchi kupata elimu sahihi juu ya sensa ya watu na makazi inayotarajiwa kufanyika mwakani ili ofisi hiyo iweze kukabiliana na baadhi ya changamoto za uwelewa mbaya wa wananchi kuhusu suala la sensa.

Alisema ni vyema wananchi wakaelimishwa ili wafahamu kwamba kushiriki katika sensa ni uwekezaji muhimu na uwekaji wa mipango sahihi ya maendeleo ya Zanzibar.

Naye Kamisaa wa Sensa Zanzibar, Balozi Mohammed Hamaza, amemweleza makamu kwamba maandalizi ya sensa hiyo yanaendelea ikiwa ni pamoja ukataji wa maeneo ya kuhesabu watu.

Balozi Hamza alisema sensa ijayo itafanyika kwa kutumia teknolojia ya kisasa ili kuwezesha kukusanywa kwa usahihi takwimu mbalimbali zinazohusu idadi ya watu, makazi, shughuli za kijamii na mambo mengine.

Katika hatua nyingine Othman alikutana na uongozi wa Chama cha Mabaharia Zanzibar na kuahidi kushirikiana na chama hicho kusaidia kutatua changamoto mbalimbali za mabaharia ikiwamo kufuatilia suala la kupatikana malipo ya fidia kwa mabaharia wa Zanzibar waliopata matatizo wakiwa kazini.

Naye Katibu wa Chama cha Mabaharia Zanzibar, Hussein Said Uki, alisema kusitishwa suala la usajili wa meli za nje Zanzibar na kukosekana chuo cha kufundisha mabaharia ni changamoto kubwa inayowakabili.

Alisema suala la usitishwaji wa usajili wa meli za kigeni Zanzibar kunaipunguzia mapato serikali na pia kuwakosesha vijana ajira.

Katibu huyo aliiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kufuatilia suala hilo la kusitishwa usajili wa meli za kimataifa Zanzibar kwa kuwa ni muhimu kwa uchumi na maendeleo ya wananchi wake.

Alisema katika kipindi ambacho Zanzibar inaendeleza harakati za uchumi wa bluu, suala la mafunzo na elimu ya ubaharia ni muhimu na hakuna budi kurejesha chuo cha mabahari kilichokuwapo awali.

## Wafurahia mradi kurudisha watoro shuleni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAFADHILI wa mradi wa kuwarejesha watoto shule, katika ngazi ya msingi, wameelezea kuridhishwa na hatua ya Wizara ya Elimu kuwarejesha shule watoto waliotoroka.

Wakizungumza wakati walipofanya ziara kuangalia baadhi ya shule waliopo wanafunzi hao walisema, juhudi kubwa bado zinahitajika kuwarejesha watoto hao hasa wanawake.

Mwakilishi kutoka taasisi ya elimu kwa wote kutoka Qatar, Mary Pigoz, alisema imeonekana idadi kubwa ya watoto waliorejea hadi sasa ni wanaume kuliko wanawake, hali inayoonyesha kuwapo kwa mwamko mdogo kwa wazazi na walezi katika kuwarejesha watoto wao shule hasa wanawake.

Aliahidi kuyafanyia kazi mahitaji yote wanayoyataka ili kuhakikisha wanawasaidia watoto hao kusoma na kuwa viongozi bora wa baadaye.

Naye Mkurugenzi Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khalid Masoud, alisema madhumuni ya ziara hiyo ni kuona kwa vitendo namna mradi huo ulivyoanza kutekelezwa tangu ulipozinduliwa na Makamu wa Pili wa Rais.

Alisema mpaka sasa wanafunzi 4,009 wamesharejeshwa shule kwa Unguja na Pemba na bado wanaendelea kuwahamasisha jamii na viongozi wa ngazi za shehia, wilaya na mikoa ili kusaidia kuwarudisha shule watoto hao.

Kwa upande wao wanafunzi wamepata nafasi ya kuiomba Wizara ya Elimu pamoja na ufadhili huo, kuwapatia sare za shule, vifaa vyote vya kusomea pamoja na kuwawekea miundombinu bora ya shule zao ili kusoma kwa ufanisi zaidi.

Shule walizotembelewa ni pamoja na Shule ya Msingi Fukuchani, Potoa na Mkokotoni.

Mradi wa kuwarejesha watoto shule unatekelezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa ufadhili wa Shirika la UNICEF pamoja na Taasisi inayoshughulikia masuala ya elimu kwa wote EAC kutoka Qatar.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Jakaya Kikwete Foundation, Vanessa Manyota, akitoa mada katika warsha ya Bima ya Afya kwa watu wote, mjini Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Aonya urasimishaji bodaboda isiwe kigezo cha uhalifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Mjiji, Rashid Simai Msaraka, amewataka waendesha bodaboda kufahamu kuwa kurasimisha mfumo wa bodaboda isiwe kigezo cha kusababisha uhalifu na kutaka wasaidie ulinzi na usalama wa nchi.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na waendesha bodaboda na Bajaji wa Wilaya ya Mjini Unguja, kikao kilichofanyika viwanja vya Maisara.

Alisema serikali haipo tayari kuona mtu kufanya uovu kupitia biashara hiyo kwa kuwa lengo la kurasimisha biashara hiyo ni kuwasaidia vijana kujiajiri.

Alisema wataweka raratibu kila anayetamani kufanya biashara hiyo kufuata utaratibu ambao utatolewa wilayani.

"Tunataka waendesha bodaboda nidhamu zao hazitiliwi shaka lazima iwe biashara ya kistarabu," alisema.

Aliongeza kuwa; "tutaliangalia suala la bodaboda kwa macho manne na tutahakikisha tunafanya ukaguzi kwa bodaboda zote na hatutaruhusu bodaboda za wizi tukigundua umenunua pikipiki ya wizi tutakushughulikia."

Alisema hapendi kuwaona waendesha bodaboda kutumika katika vitendo vya kihalifu na kuwasisitiza kuifanya biashara hiyo yenye nidhamu.

Aliwataka wafanyabiashara hao kuwa wasafi wa mwili na kuipenda kazi yao na kuona kama kazi zingine.

Aliwatahadharisha kukaa mbali na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na kujiepusha na vitendo vya udhalilishaji na uhalifu ambavyo vinaweza kuwaweka pabaya.

Issa Khamis Juma, Mkuu wa Usalama Barabarani Wilaya ya Mjini, aliwataka waendesha bodaboda kufuata sheria ikiwamo uvaaji wa kofia ngumu kwa dereva na mteja wake.

Alisema madereva bodaboda wengi hawana leseni na kuwataka kutafuta ili kuepuka kukwazana na askari wa usalama barabarani. Hassan Vuai Hassan Mwanasheria wa Mamlaka ya Usafiri wa Barabarani, aliwataka kufuata sheria na kanuni za urasimishaji wa biashara hiyo.

Kwa upande wao waendesha bodaboda wameomba serikali kuwapunguzia masharti ya kupata leseni na kuwaruhusu kupeleka abiria bandarini na ndani ya Mji Mkongwe.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ENEO LA UWEKEZAJI LINAUZWA

LIPO KIBAHA, KONGOWE CENTRE. NI EKARI NNE,KUNA MAJENGO,UMEME NA MAJI VIPO,LINA HATI

**MAWASILIANO:**
**0713 515744**
**0657 585952**

116421402

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.256/2021**

Ombi la **UPENDO HANS MHALILA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **HANS MWANAMHALALA MHALILA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 29/09/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 24/08/2021**

116423402

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAMARES AINEA MSAKI** anatangaza kupotelewa na cheti cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0567-020** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule/chuo ya **MHONDA CENTRE** mwaka **1989**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **REF NO.BNG/RB/2385/2021**

116423502

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JULIETH HEAVENLIGHT MINJA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0205/0086** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **KIBOSHO GIRLS** mwaka **2015**,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/CHU/RB/415795/2021**

116421302

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISC.LAND APPLICATION NO.3 OF 2021**
***(emanating from Misc.land application no.2 of 2021)***
**BETWEEN**
**HALIDAY NAJEEB……..APPLICANT**
**VERSUS**
**MOHAMED A.SHATRY…….1st RESPONDENT**
**SIFA MWITU……………2nd RESPONDENT**
**ERICK AUCTION MART…………..3rd RESPONDENT**
**SUMMONS FOR APPLICATION**
**TO.MANAGING DIRECTOR ,**
**ERICK AUCTION MART AND COURT BROKER**
**P O BOX**
**DAR ES SALAAM**

**WHEREAS,** the above mentioned case has been fixed for hearing 16th day of **September ,2021 at 9:00** am before **Hon.DR.J.L.MASABO-judge** you are required to appear in this court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.
**TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that day aforementioned, the suit will be heard and determined in your absence
GIVEN under my **HAND** and **SEAL** of court this **18th day of august, 2021**

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM

116423602

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**(DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY)**
**AT DAR ES SALAAM**
**MISC.LAND APPLICATION NO.3 OF 2021**
***(emanating from Misc.land application no.2 of 2021)***
**BETWEEN**
**HALIDAY NAJEEB……..APPLICANT**
**VERSUS**
**MOHAMED A.SHATRY…….1st RESPONDENT**
**SIFA MWITU……………2nd RESPONDENT**
**ERICK AUCTION MART…………..3rd RESPONDENT**
**SUMMONS FOR APPLICATION**
**TO,SIFA MWIWU,**
**P O BOX**
**DAR ES SALAAM**

**WHEREAS,** the above mentioned case has been fixed for hearing 16th day of **September ,2021 at 9:00** am before **Hon.DR.J.L.MASABO-judge** you are required to appear in this court without fail and must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that day aforementioned, the suit will be heard and determined in your absence
**GIVEN** under my **HAND** and **SEAL** of court this 18th day of **august, 2021**

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
DAR ES SALAAM

116423802

---

KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD
COURT BROKER

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 24/09/2021 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA TOYOTA ALTEZA T 839 DJX, MALI YA ZAKAYO AYIEKO CYPRIAN, BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LIMITED, P.O. BOX4169 DODOMA. MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0688729841/0784718272.**

116424702

---

KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD
COURT BROKER

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

TUTAFANYA MNADA TAREHE 24/09/2021 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA GARI AINA YA FORD ESCAPE T 565 CXL, MALI YA MWELLA YUSUF MAKWAIA, BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA IMARISHA MAISHA LIMITED, P.O. BOX4169 DODOMA. MNADA UTAFANYIKA NYERERE SQUARE, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0688729841/0784718272.**

116424702

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.80 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PHILIPO BETHSEBA CHELELO**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY NEEMA ROBERT SANGA.**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the **29 Day of SEPTEMBER 2021.**
**Dated at Dodoma this 23rd day of August 2021.**

MAGISTRATE

116424802

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SAMSON MENAS KALO** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari aina ya **SUZUKI CARRY** yenye namba za usajili **T 895 DGD Chassis No. DC51T542493, Engine No.4555457.**Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi **DOD/DOD/RB/414122/2021.**

116424902

---

# FOR SALE



Embassy of the State of Qatar in Dar es Salaam would like to sale **2012 TOYOTA HILUX PICK-UP in a mint condition.**

Interested buyers can view the vehicle between **0900-1500 at the Embassy located at 6 Msasani Road, Dar es salaam.**

116422702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Wilaya ya DODOMA**
**MADAI NAMBARI 92/2021**
**MDAI GEOFREY IBRAHIMU**
**DHIDI YA**
**MDAIWA ANJELICK MZIRAYI**
**Kwa ANJELICK MZIRAYI**
**MOSHI.**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba **MADAI TSH 755,000/=**
Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya **JUMANNE Tarehe 31/08/2021 saa 2.30 asubuhi** kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kuitwa shauri hilo ni lazima kuleta mashidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo **tarehe 24/08/2021.**

116424402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**
**Mahakama ya mwanzo ya maili moja**
**Wilaya ya kibaha**
**MADAI NAMBARI 90 ya 2020**
**Mdai….Twahili Kasimu**
**Mdaiwa…..Emanuel Makota**
**Kwa.Twahili kasimu kwa mfipa 0714330060**

Kwakua mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba ….utekelezaji

Kwahiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii jumatano tarehe 08/09/2021 saa 2:00 asubuhi kwakujibu madai hayo na kwakua siku hiyo nisiku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwaajili ya kujitetea kaika shauri hilo
**Angalia,** kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii,itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 28/07/2021

116422002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA.111 YA MWAKA 2021**
**BAINA YA**
**JOVINARY WILFRED RWEMIGIRA …… MKAZA HUKUMU**
**DHIDI YA**
**ISAKA NYAU NA WNZAKE………WAKAZIWA HUKUMU**

**KWA:**
**ELIA CHIBADA**
**ALFONCE PAULO MAYUNGA**
**GRACIANA LANDANI MWAMBANDALE**
**POPOTE MLIPO.**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili. Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi,Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa Kisheria tarehe **07.09.2021** saa 3.00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo unatakiwa kuleta utetezi wako kwa maandishi.
**ANGALIZO:** - Kama haukuhudhurisa tarehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa umepokea Hati ya Wito, Baraza linaweza kutoa HJukumu dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04 ya Mwezi Agosti,2021.

116422302

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**HILDA FREDY ZANDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0938/0029** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary MBEZI BEACH HIGH mwaka 2018,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **WMB/RB/417/2021**

116421202

---

## NAFASI ZA KAZI

**A SALES PERSON IS REQUIRED**
A SALES PERSON IS REQUIRED FOR AN ESTABLISHED PHARMACEUTICAL COMPANY BASED IN DAR ES SALAAM
**CONTACT: 0713 786 300**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha DODOMA Mkoa DODOMA**
**Shauri la madai No……. /2021**
**Jina la mdai DICKSON KATANGA**
**Jina la mdaiwa JUMA SALMIN**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa JUMA SALMIN**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba MADAI YA PESA TSH 2,900,000.**

Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 30 mwezi 08 mwaka 2021 saa 2:00 asubuhi. Kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinazohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na kuthibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo **20/08/2021.**

HAKIMU
PRINCIPAL
COURT MAGISTRATE

116424602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya wilaya ya njombe**
**Kituo cha njombe mjini Mkoa wa njombe**
**Usimamizi wa mirathi na 12/2019**
**Godfrey Thomas mfyuji……..marehemu**
**Thomas godfrey mfyuji……..mwombaji**

**TAARIFA KWA UMMA**
**MAOMBI YA KUTANGAZA KUFUNGA MIRATHI**

Kwa watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi

Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 25th ya mwezi wa September 2021

**Imetolewa na hakimu mkazi leo siku ya tarehe 24th agosti mwaka 2021**

HAKIMU MKAZI

216424501

---

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Chad kutofanya mazishi ya Rais wa zamani Hissen Habre

**N'Djamena, CHAD**

SERIKALI ya Chad imesema haina mpango wa kuandaa mazishi ya kitaifa kwa aliyekuwa rais wa Hissene Habre, aliyefariki dunia siku ya juzi, baada ya kuambikizwa virusi vya corona, nchini Senegal akitumikia kifungo cha maisha kwa uhalifu dhidi ya binadamu.

"Kufuatia uhalifu wake na kutowaheshimu waathiriwa wa vitendo vyake vya uhalifu, hakutokuwa na sherehe rasmi za kumuenzi", serikali ya Chad imeliambia shirika la habari la AFP.

Kiongozi huyo wa zamani wa Chad, alifariki katika hospitali kuu mjini Dakar, juzi, akiwa na umri wa miaka 79.

Habre alichukua madaraka mwaka wa 1982, akiiongoza Chad kimabavu hadi alipokimbilia Senegal, mwaka wa 1990 baada ya kuondolewa madarakani na Idriss Deby Itno.

Uongozi wake uligubikwa na ukandamizaji wa kikatili dhidi ya wapinzani, ikiwamo madai ya mateso na mauaji holela ya wapinzani, huku watu 40,000 wanakadiriwa kuuawa, vitendo vilivyosababisha Habre kupewa jina la utani la "Pinochet wa Afrika".

**VOA**

## Algeria yavunja uhusiano wa kidiplomasia na Morocco

**Rabat, MOROCCO**

WAZIRI wa Mambo ya Kigeni Algeria Ramtane Lamamra, amesema kwamba taifa lake limevunja uhusiano wa kidiplomasia na Morocco, wakati uhusiano kati ya mataifa mengi ya Afrika Kaskazini ukiendelea kudorora.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AP Lamamra, kuhusu taarifa ya rais kuhusiana na hatua hiyo.

Tangazo hilo limekuja baada ya karibu wiki moja tangu rais wa Algeria Abdelmadjid Tebboune, kulieleza baraza la usalama kuhusu uchokozi wa Morocco, wakati akisisitiza umuhimu wa kutathmini tena uhusiano wa mataifa yote mawili, pamoja na haja ya kuimarisha usalama kwenye mpaka wao.

Algeria na Morocco, kwa muda mrefu wameishi katika mazingira ya mivutano huku wakiwa wamefunga mipaka baina yao.

Hali ilidorora zaidi wiki kadhaa zilizopita baada ya balozi wa Morocco kwenye Umoja wa Mataifa kusema kwamba, watu wa Algeria kwenye eneo la Kabyle wanastahili kupewa nafasi ya kuamua hatima yao.

Algeria imekuwa ikiunga mkono kundi la wapiganaji wa Polisario, ambalo linadai kujitawala kwa eneo hilo lililotekwa na Morocco mwaka 1975.

**VOA**

# Uganda, Rwanda zapokea wakimbizi kutoka Afghanistan

**Kampala,** UGANDA

WIZARA ya Mambo ya Nje Uganda imesema kundi la kwanza la wakimbizi 51 kutoka Afghanistan, limewasili jana asubuhi katika uwanja wa kimataifa wa Entebbe kupitia ndege binafsi.

Wizara hiyo imeongeza kwamba, kundi hilo linapita tu Uganda na litaelekea Marekani na nchi nyingine, ingawa haijafahamika kundi hilo litakaa Uganda kwa muda gani.

Watu hao walifanyiwa vipimo vya virusi vya corona na watakaa karantini, taarifa hiyo imesema.

Uganda ilipokea watu hao kufuatia maombi ya serikali ya Marekani ya kutaka nchi hiyo isaidie kupokea watu wanaokimbia ghasia za Afghanistan, tangu kundi la Taliban lishike hatamu juma lililopita.

Wiki iliyopita serikali ya Uganda iliiambia BBC kwamba, nchi hiyo inatarajia kupokea wakimbizi 2,000 kutoka Afghaistan, kutokana na maombi ya Marekani.

Maofisa wa juu wa serikali baadae walisema mazungumzo bado yanaendelea.

Uganda inawahifadhi wakimbizi zaidi ya milioni moja, kutoka nchi za ukanda wa Afrika Mashariki ambao wamekimbia nchi zao, kwa sababu ya vita na majanga mengine.

Rwanda itakuwa mwenyeji wa wasichana wengi wa shule wanaohamishwa kutoka Afghanistan kufuatia kuchukuliwa kwa nchi hiyo na wanamgambo wa Taliban. Shabana Basij-Rasikh, mwanzilishi wa Shule binafsi ya Uongozi Afghanistan (SOLA), alisema jana kwamba, wanafunzi wapatao 250, wafanyakazi na wanafamilia walikuwa njiani kwenda Rwanda, kupitia Qatar, kuanza muhula mwingine kwa wanafunzi wote.

Wizara ya Elimu Rwanda, ilituma ujumbe wa kukaribisha jamii ya SOLA.

Mwanzilishi wa shule hiyo alisema walikuwa na matumaini ya kuishi kwa muda tu hadi muhula ukamilike na kurudi Afghanistan wakati hali itakapokuwa tulivu . Waafghanistan wamekuwa wakikimbia kuondoka nchini mwao, kwa hofu ya kuishi chini ya utawala wa Taliban na maelfu wamehamishwa kwenda nchi zingine.

Marekani na baadhi ya washirika wake, wameshindwa kuafikiana juu ya msimamo wa Rais Joe Biden wa kusisitiza Agosti 31, kama muda wa mwisho wa kuondoa vikosi vyake vya usalama Afghanistan, hatua ambayo itafunga kabisa zoezi la kuwahamisha watu kutoka Kabul.

**BBC/DW**



Baadhi ya Waafghanistan wakiwasili mjini Roma, jana, wakitokea Kabul kwa ajili ya hifadhi, pichani mtoto akiwa ameketi chini kwenye Uwanja wa Ndege wa Fiumicino Italia. **PICHA: REUTERS**

# Taliban yatoa agizo wanawake wafanyakazi kubaki nyumbani

**Kabul,** AFGHANISTAN

WANAWAKE wanaofanya kazi Afghanistan, kwa lazima wametakiwa kubaki nyumbani hadi mifumo sahihi itakapowekwa, kuhakikisha usalama wao, msemaji wa Taliban amewaambia waandishi wa habari.

"Ni utaratibu wa muda mfupi," msemaji Zabihullah Mujahid alisema. Taliban, ambao walitekeleza sharia kali za kiislamu wakati walipokuwa wakiongoza Afghanistan kabla ya 2001, walichukua udhibiti kamili wa nchi hiyo, siku 10 zilizopita.

Umoja wa Mataifa (UN), unafuatilia ripoti za kuaminika kuhusu dhuluma za Taliban, hasa vikwazo dhidi ya wanawake.

Kamishna Mkuu wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa Michelle Bachelet, alisema jana kwamba haki za wanawake ni mstari mwekundu ambao Taliban hawafai kuuvuka.

Katika mkutano wake na waandishi wa habari, Kabul, msemaji wa Taliban, pia alizungumzia uokoaji unaoongozwa na Marekani kutoka Mji Mkuu, Kabul.

**BBC**

## Kenya, Tanzania kuondoa vikwazo kibiashara Desemba mwishoni

**Nairobi,** KENYA

KENYA na Tanzania, zimekubaliana kufikia Desemba, mwaka huu, ziwe zimeondoa vikwazo vya kibiashara visivyo vya kikodi baina ya nchi mbili.

Makubaliano hayo yamefikiwa katika kikao cha pamoja kati ya vyombo vilivyoundwa kushugulikia masuala yanayoathiri ushirikiano, hasa wa kibiashara baina ya nchi mbili.

Mkutano huo wa siku tano uliofanyika Nairobi na kumalizika juzi, umefikia makubaliano ya kuondoa vikwazo vilivyokuwa vinaikumba mara kwa mara biashara za nchi hizo, ili kuongeza ufanisi wa shughuli za kibiashara zinazovuka mipaka.

Juni mwaka huu, mwezi mmoja baada ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan nchini Kenya, kamati iliyoundwa ilibainisha changamoto zaidi ya 60 za kikodi za zisizo za kikodi, zinazozikabili nchi hizo, ikiwamo tozo za ukaguzi wa bidhaa mipakani.

Taarifa ya pamoja kutoka kikao hicho, zinasema changamoto 30 kati ya 64 zimeshafanyiwa kazi, huku zilizosalia zikifanyiwa kazi kabla ya Desemba mwaka huu.

**BBC**

MECHI KALI
HOME
AWAY
HJK HELSINKI
3.49 | 3.39 | 2.09
FENERBAHCE

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
halopesa
SEND

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 450



# MADRID YAKARIBIA KUMNASA MBAPPE

**MADRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe amekuwa akihusishwa kuhamia Real Madrid kwa miaka sasa, lakini angalau inaonekana sasa yupo karibu kujiunga na Los Blancos hao kuliko wakati wowote ule.

Mbappe amekataa kusaini mkataba mpya na PSG na mkataba wake wa sasa unamalizika majira ya joto mwakani.

Kwa mujibu wa ripoti ya RMC Sport, PSG sasa inazingatia uwezekano wa kumuuza Mbappe kabla ya dirisha la usajili halijafungwa.

Kwa kushangaza, kama Mbappe atahamia Real Madrid, inaweza kuwa na athari kwa mustakabali wa mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo, ambaye ghafla anaweza kuwa chaguo kwa PSG.

Real Madrid wamebaki wakisisitiza kwamba, wanafikiria tu kumsajili Mbappe, licha ya kuwa na chaguo la kwenda kwenye njia ya kujadili makubaliano na mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland au hata hatua ambayo itamfanya Ronaldo arejee pale Santiago Bernabeu.

Hata hivyo, kocha wa Madrid, Carlo Ancelotti mapema wiki iliyopita alibainisha wazi kuwa, hana mpango na Ronaldo kwenye kikosi chake.

# Arteta: Itachukua muda Arsenal kurejea sawa

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amekubali "itachukua muda" kwa Arsenal kurudi katika kiwango chake baada ya klabu hiyo kuwa na mwanzo mbaya zaidi kwenye Ligi Kuu England katika historia yake.

Washikabunduki hao walipoteza mabao 2-0 kwa Brentford na Chelsea kwenye mechi zake mbili za mwanzo za msimu huu na wapo kwenye mstari wa kushuka daraja baada ya mechi mbili, ikiwa ni mara ya kwanza tangu Agosti mwaka 1992.

Arsenal walimaliza Ligi Kuu England msimu uliopita wakiwa katika



nafasi ya nane na hawakufuzu kucheza michuano ya Ulaya.

Na sasa Kocha Arteta, ambaye sasa amekalia kuti kavu amebainisha wazi kuwa, itachukua muda timu hiyo kurudi kwenye kiwango chake.

"Naweza kusema asanteni kwa sababu hali ya timu nilivyoiona kabla ya mchezo wa Chelsea ilikuwa ya aina yake," alisema Arteta.

"Mambo yamekuwa tofauti, timu ilijitahidi kwa kadili ilivyowezа, lakini vitu havikuwa sawa.

"Mashabiki walijaribu kuipa sapoti timu yao, na wachezaji wanajua wanawakatisha sana tamaa mashabiki wanapopoteza nyumbani."

## HABARI MICHEZO


,150,500 JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/08/21 | 17:00 | Brighton vs Everton | 2.31 | 3.27 | 3.16 |
| 02. 28/08/21 | 17:00 | Newcastle vs Southampton | 2.60 | 3.40 | 2.65 |
| 03. 28/08/21 | 17:00 | Huddersfield vs Reading | 2.42 | 3.20 | 2.86 |
| 04. 28/08/21 | 17:00 | Preston vs Swansea | 2.46 | 3.26 | 2.77 |
| 05. 28/08/21 | 17:00 | Luton Town vs Sheffield Utd | 2.87 | 3.11 | 2.47 |
| 06. 28/08/21 | 18:00 | Celta Vigo vs Athletic Bilbao | 2.42 | 3.22 | 3.02 |
| 07. 28/08/21 | 19:30 | Liverpool vs Chelsea | 2.45 | 3.36 | 2.86 |
| 08. 28/08/21 | 20:30 | Real Oviedo vs Tenerife | 2.60 | 2.85 | 2.95 |
| 09. 29/08/21 | 16:00 | Burnley vs Leeds | 3.11 | 3.41 | 2.27 |
| 10. 29/08/21 | 16:00 | Angers vs Rennes | 2.85 | 3.20 | 2.50 |
| 11. 29/08/21 | 16:30 | Union Berlin vs Monchengladbach | 2.69 | 3.19 | 2.64 |
| 12. 29/08/21 | 20:30 | Cadiz CF vs Osasuna | 3.01 | 3.01 | 2.56 |
| 13. 29/08/21 | 20:30 | Rayo Vallecano vs Granada | 2.61 | 3.22 | 2.77 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 26 - AGOSTI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:30 | 2509 | Ufa vs Kryliya Sovetov | 2.81 | 3.05 | 2.56 |
| 17:00 | 2498 | Kairat Almaty vs Fola | 1.29 | 5.24 | 7.76 |
| 17:00 | 3329 | Fernando Mora vs CA 3 De Febrero | 2.18 | 3.04 | 3.24 |
| 17:00 | 3812 | Pakhtakor vs Otmk Olmaliq | 1.32 | 4.67 | 7.98 |
| 17:00 | 5860 | Dinamo-Auto vs Zimbru | 2.47 | 3.64 | 2.41 |
| 17:00 | 5948 | Deportivo Capiata vs Atyra FC | 2.56 | 3.05 | 2.66 |
| 18:00 | 1975 | Tsarsko Selo vs Botev Plovdiv | 2.46 | 3.14 | 2.70 |
| 18:00 | 2907 | Alashkert Martuni vs Rangers | 6.20 | 4.40 | 1.49 |
| 18:15 | 3560 | Al Dhafra vs Al Sharjah SC | 6.39 | 4.84 | 1.37 |
| 18:15 | 4306 | Al Nasr Dubai vs AL Urooba | 1.27 | 5.59 | 7.71 |
| 18:30 | 1364 | Manama Club vs East Riffa | 2.80 | 3.09 | 2.41 |
| 18:30 | 2911 | Spartak Moscow vs Sochi | 1.76 | 3.60 | 4.34 |
| 18:30 | 4432 | AL Khalidiyah vs AL Badii | 2.31 | 3.25 | 2.82 |
| 18:30 | 5845 | Santos FC Ica vs Molinos EL Pirata FC | 2.07 | 3.48 | 3.09 |
| 18:45 | 4259 | Al Fateh (KSA) vs Al Shabab Riyadh | 3.50 | 3.70 | 1.94 |
| 19:00 | 2231 | HJK Helsinki vs Fenerbahce | 3.49 | 3.39 | 2.09 |
| 19:00 | 4270 | Lincoln FC vs FC Riga | 2.99 | 3.13 | 2.27 |
| 19:00 | 4553 | Ullensaker/Kisa vs Bryne | 2.51 | 3.43 | 2.47 |
| 19:00 | 5248 | Bodo Glimt vs Zalgiris | 1.20 | 5.96 | 10.57 |
| 19:00 | 5776 | MSK Zilina vs Baumit Jablonec | 2.60 | 3.71 | 2.27 |
| 20:00 | 1280 | CSKA Sofia vs Viktoria Plzen | 2.35 | 3.19 | 2.81 |
| 20:00 | 1802 | GD Chaves vs Viseu | 1.66 | 3.48 | 5.09 |
| 20:00 | 2091 | Elfsborg vs Feyenoord | 3.82 | 3.58 | 1.81 |
| 20:00 | 4384 | Hammarby vs FC Basel | 3.29 | 3.53 | 1.97 |
| 20:15 | 2673 | Godoy Cruz vs Union Santa Fe | 2.39 | 3.00 | 2.91 |
| 20:30 | 1310 | Akhmat Grozny vs Arsenal Tula | 1.79 | 3.71 | 4.05 |
| 20:30 | 3890 | Maccabi Tel Aviv vs Shakhter Karagandy | 1.20 | 5.63 | 11.64 |
| 20:45 | 1116 | Zenit St Petersburg vs CSKA Moscow | 1.54 | 4.32 | 5.11 |
| 20:45 | 5230 | Al Nasr Riyadh vs Al Taawon | 1.38 | 5.15 | 6.73 |
| 21:00 | 1638 | HNK Rijeka vs PAOK | 3.48 | 3.43 | 1.94 |
| 21:00 | 2194 | La Serena vs Audax Italiano | 2.80 | 3.29 | 2.30 |
| 21:00 | 2271 | St Johnstone vs LASK Linz | 3.35 | 3.30 | 2.03 |
| 21:00 | 2972 | Galatasaray vs Randers | 1.58 | 4.11 | 5.41 |
| 21:00 | 3734 | KAA Gent vs Rakow Czestochowa | 1.31 | 4.63 | 8.50 |
| 21:00 | 4618 | Al Hidd Club vs Al Hala Muharraq | 1.56 | 4.06 | 4.84 |
| 21:15 | 1051 | AZ Alkmaar vs Celtic | 2.22 | 3.86 | 2.86 |
| 21:15 | 5367 | Union Berlin vs KuPS Kuopio | 1.12 | 7.33 | 15.43 |
| 21:30 | 4596 | CFR Cluj vs Red Star Belgrade | 2.96 | 3.26 | 2.41 |
| 21:45 | 5418 | Slovan Bratislava vs Olympiakos | 3.70 | 3.70 | 1.92 |
| 21:45 | 5609 | Shamrock Rovers vs Flora Tallinn | 1.69 | 3.83 | 4.16 |
| 21:45 | 5621 | Aberdeen vs Karabakh | 2.09 | 3.19 | 3.29 |
| 22:00 | 1355 | Legia Warszawa vs Slavia Prague | 3.30 | 3.55 | 2.11 |
| 22:00 | 2388 | Partizan vs Santa Clara | 1.84 | 3.44 | 3.83 |
| 22:00 | 3499 | Talaea El Gaish vs Al Masry Club | 2.48 | 3.37 | 2.67 |
| 22:00 | 3773 | Royal Antwerp vs Omonia Nicosia | 1.56 | 4.17 | 5.57 |
| 22:00 | 3950 | Sturm Graz vs NK Mura | 1.24 | 5.98 | 11.96 |
| 23:00 | 2474 | Mineros Guyana vs Lala FC | 1.89 | 3.88 | 3.25 |
| 23:30 | 1303 | KFG vs Hottur | 2.16 | 3.72 | 2.76 |
| 23:30 | 2733 | Santiago Wanderers vs Union Espanola | 3.01 | 3.20 | 2.22 |
| 23:30 | 5422 | Deportivo Llacuabamba vs Juan Aurich | 3.29 | 3.53 | 1.97 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MAN CITY YATAJA DAU LA LAPORTE




**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City imetaja dau la fedha wanayotaka ili kumwachia, Aymeric Laporte, kwa mujibu wa Daily Mail.

Manchester City wametaja kiasi cha pauni milioni 60 ndio kinaweza kumtoa beki huyo wa Hispania ambaye inasemekana hana furaha kutokana na kukosa nafasi ya kucheza katika kikosi hicho.

Mabingwa wa hao wa Ligi Kuu England watasikiliza dau lenye thamani ya kuanzia pauni milioni 60 au zaidi kwa Laporte, ambaye msimu uliopita alicheza mbele ya Ruben Dias na John Stones kwenye safu ya ulinzi.

Klabu za Juventus na Real Madrid hivi karibuni zimehusishwa na mpango wa kuwania huduma ya beki huyo wa kati, lakini hadi sasa hakuna ofa rasmi iliyowakilishwa katika klabu ya City.

Taarifa za karibu zinasema Laporte anapata shida kupata timu nyingine kutokana na mshahara mkubwa anaolipwa na City wa pauni milioni 160,000 kwa wiki.

Hata hivyo, Laporte anaweza kutua Juventus kama dili la Cristiano Ronaldo litakamilika kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili la kipindi hiki cha majira ya joto.

City, imeripotiwa ikimtaja Laporte au Bernardo Silva mmoja wao kutumika kwenye dili la kumsajili Ronaldo.

# *Fati arejea mazoezini Barcelona*



**BARCELONA, Hispania**

FOWADI wa Barcelona, Ansu Fati amerejea mazoezini na kikosi cha kwanza baada ya kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu kutokana na majeraha.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 alikosa nusu ya pili ya msimu wa LaLiga baada ya kuumia goti la upande wa kushoto hapo Novemba, mwaka jana.

Fati alipata jeraha wakati wa ushindi wa 5-2 wa Barcelona dhidi ya Real Betis huko Camp Nou, na baadaye akafanyiwa operesheni tatu.

Lakini, mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania anakaribia kurudi uwanjani baada ya kupigwa picha tena kwenye uwanja wa mazoezi wa Barcelona, Ciutat Esportiva Joan Gamper siku ya Jumanne.

Ingawa hatapatikana kwenye mchezo wa LaLiga wa wikendi hii dhidi ya Getafe, Fati anaweza kuwa kwenye safari ya Barcelona kwenda Sevilla Septemba 11, mwaka huu. Fowadi huyo alikua mfungaji mwenye umri mdogo zaidi katika historia ya Barca wakati alipofunga dhidi ya Osasuna Agosti 2019 akiwa na miaka 16 na siku 304.

Fati ameongeza mabao mengine 12 katika mechi 42 kwenye mashindano yote ya Blaugrana hao, ambayo alijiunga nayo akiwa na umri wa miaka 10.

Kijana huyo aliyezaliwa Guinea-Bissau amecheza mara nne na timu ya taifa ya Hispania, na alifunga bao lake la kwanza la kimataifa dhidi ya Ukraine Septemba, 2020.

## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RONALDO ALAZIMISHA KURUDI KATIKA EPL

●●● Mshambuliaji huyo kutoka Ureno ameweka wazi kuwa hataki...

**TURIN, ITALIA**

CRISTIANO Ronaldo anataka kulazimisha uhamisho wa kwenda kwenye Ligi Kuu ya England, kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili wa kipindi hiki cha majira ya joto, kwa mujibu wa L'Equipe.

Uvumi umekuwa ukisambaa kwa muda sasa kuhusu majaliwa ya Ronaldo pale Juventus.

Ronaldo aliwekwa benchi kwenye mchezo wa kwanza wa Juventus wa ufunguzi wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Jumapili.

Kocha wa Juve, Massimiliano Allegri alisisitiza kuwa hakukuwa na kitu chochote kilichosababisha asicheze, lakini uvumi umeendelea kukua tangu hapo.

Raia huyo wa Ureno na fowadi wa zamani wa Manchester United anataka kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Manchester City, huku ripoti ikimtaja Aymeric Laporte au Bernardo Silva mmoja wao kutumika kwenye dili hilo.

Ronaldo ameripotiwa kwamba hataki kumalizia mwaka wake mmoja kwenye mkataba aliobakia hapo Juventus, huku uvumi ukisema kwamba, jambo lake linaweza kumalizwa wiki hii.

Sky Sport Italia imedai kwamba, Ronaldo amefanya mawasiliano kuhusu mpango wake huo na wachezaji wa Juve na Man City.

Ronaldo amecheza kwa kipindi cha misimu mitatu kule Juventus baada ya kutamba sana Real Madrid.

## ZISIKUPITE

### MADRID WATUMA OFA
REAL Madrid imepeleka ofa ya kwanza ya pauni milioni 137 kwa ajili ya mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22, lakini klabu hiyo ya Ufaransa inatarajia kukataa ofa yoyote kwa ajili ya nyota huyo aliyebakiza mkataba wa mwaka mmoja. ***(Mail)***

### PSG YAMTAKA RICHARLISON
KLABU ya PSG inaweza kumwania mshambuliaji wa Everton na Brazil, Richarlison mwenye umri wa miaka 24, kama mbadala wa Mbappe. ***(Eurosport)***

### RONALDO KUSHAWISHI
MSHAMBULIAJI wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, atashawishi ahamie kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Manchester City katika wiki hii ya mwisho ya usajili, huku nyota huyo wa zamani wa Manchester United angetamani kutomalizia mkataba wake wa mwaka mmoja uliosalia hapo Turin. ***(L'Equipe)***

### WACHEZAJI NA CORONA
KLABU za Ligi Kuu ya England hazitawaruhusu wachezaji wake kuchezea timu zao za taifa katika mataifa yenye hatari kubwa ya maambukizi ya virusi vya corona.***(Mail)***

### HAALAND ANUKIA MAN UNITED
KLABU ya Manchester United ipo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland msimu ujao. Kinda huyo mwenye miaka 21 amekuwa lulu sokoni baada ya kufunga mabao 62 katika mechi 63 alizowachezea Wajerumani hao wa ligi ya Ujerumani, Bundesliga.***(Bild)***

### NUGUEZ AGOMBEWA EPL
CHELSEA huenda ikakabiliana na Manchester United kama watajitosa kujaribu kunasa saini ya kiungo wa Atletico Madrid na Hispania, Saul Niguez kwenye umri wa miaka 26. ***(Guardian)***

### SARABIA NA NIGUEZ
KAMA kiungo, Saul Niguez ataondoka Atletico Madrid, klabu hiyo imemworodhesha kiungo wa Hispania, Pablo Sarabia kutoka Paris St-German kama mbadala wake. ***(Marca)***

### TRIPPIER AITAKA MAN UNITED
ARSENAL imefanya mazungumzo na Atletico Madrid kuhusu uhamisho wa beki wa kulia wa England, Kieran Trippier, ingawa beki huyo mwenye umri wa miaka 30 angetamani kwenda Manchester United kama atatakiwa kuondoka Madrid.***(Marca)***

### NYOTA KUTEMWA ARSENAL
WINGA wa Brazil, Willian mwenye umri wa miaka 33, beki wa kulia wa England, Ainsley Maitland-Niles mwenye miaka 23, mshambuliaji, Eddie Nketiah mwenye miaka 22, Hector Bellerin (26), Lucas Torreira (25), Reiss Nelson (21) na Sead Kolasinac (28) huenda wakatupiwa virago na Arsenal wiki ijayo. ***(Standard)***

### ZOUMA HUYO WEST HAM
WEST Ham wana matumaini ya kumsajili mlinzi wa kati wa Ufaransa, Kurt Zouma kutoka Chelsea kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili. ***(Telegraph)***

HABARI MICHEZO

## Azam FC, Zanaco kupimana ubavu

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Yanga ikitarajia kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya Zanaco kutoka Zambia katika kiilele cha Wiki ya Mwananchi itakayochezwa keshokutwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, Azam yenyewe itavaana na vigogo hao katika mechi zake nne za kirafiki watakazocheza wakiwa nchini Zambia.

Azam FC imeweka kambi Zambia kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat', amesema kikosi hicho kitakaa Zambia kwa siku 12, na kimeshaanza kufanya mazoezi mara mbili asubuhi na jioni, huku kikitarajia kucheza mechi nne za kurafiki kabla ya kurejea Tanzania.

Popat alisema wanaamini mechi hizo zitasaidia kuwaimarisha wachezaji wao na kuwa tayari kukabiliana na ushindani katika msimu mpya utakaoanza Septemba 25, mwaka huu.

"Kikosi kitakaa kwa siku 12, mazoezi kinafanya mara mbili kwa siku na kitacheza mechi nne, kila baada ya siku mbili, na ni dhidi ya Zanaco, Zesco, Red Arrow na Forest Ranger," Popat alisema.

## Dube arejea dimbani kamili

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa Azam FC, Price Dube ameanza mazoezi 'makali' baada ya kutoka katika majeruhi na amejiunga na kikosi cha timu hiyo kilichoweka kambi yake kwenye Mji wa Ndola, Zambia.

Azam FC imeweka kambi nchini humo kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya hatua ya awali ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Horseed SC ya Somalia.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati alisema Dube wanafuraha kuona mshambuliaji huyo amerejea kikosini kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya ambao wanakabiliwa na mashindano mbalimbali.

"Hakuweza kumaliza mechi za msimu uliopita kwa sababu alipewa mapumziko ya wiki mbili ili kuhakikishia amepona kwa asilimia kubwa, tunashukuru yuko fiti na tayari kuendelea na majukumu yake ya kazi," alisema Vivier.

Kocha huyo alisema wanatarajia kumpa dakika chache katika mechi za kirafiki watakazocheza ili kuendelea kumjenga taratibu.

"Tunajua (modern football), kucheza na mtu haumjuwi ni shida kubwa sasa kwa hiyo ni lazima tutafute habari za wapinzani ikiwamo ubora na madhaifu yao, tuna imani na wao wenyewe wanatafuta kujua habari zetu," alisema kocha huyo.

# SAMATTA KUJIUNGA NA TAIFA STARS J'PILI DRC

**Na Tunu Hassan, TUDARCo**

MSHAMBULIAJI na nahodha wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samata anatarajiwa kujiunga na kikosi hicho jijini Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Jumapili kwa ajili ya mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia dhidi ya wenyeji itakayochezwa Septemba 2, mwaka huu.

Taifa Stars imepangwa Kundi J pamoja na DRC, Madagascar na Benin.

Katika kujiandaa na mechi hiyo na nyingine dhidi ya Madagascar itakayochezwa Septemba 7, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, Stars iliingia kambini juzi.

Samatta atajiunga na kikosi hicho siku ya Jumapili akitokea nchini Uturuki, ili kujiandaa na mchezo wa kwanza dhidi ya DR Congo Septemba 2 na ule wa Septemba 7, mwaka huu dhidi ya Madagascar.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jijini jana, Mratibu wa Taifa Stars, Danny Msangi alisema maandalizi yanaendelea vizuri chini ya Kocha Kim Poulsen na wachezaji wote wanaonyesha ari ya kujituma ili kuhakikisha wanapata mafanikio katika mechi hizo.

Msangi alisema Samatta atajiunga na kikosi hicho Jumapili mjini Lubumbashi wakati winga, Simon Msuva ambaye anacheza soka la kulipwa nchini Morocco atajiunga na wenzake Jumamosi.

"Ni kweli timu ipo salama na wachezaji wote wana ari kubwa ya kufanya vizuri na matumaini ni makubwa ya vijana kupambana na kufanikiwa kufika mbali zaidi, tunaamini wataitendea haki jezi ya Timu ya Taifa," alisema Msangi.

Aliongeza kila kitu kwenye kambi hiyo kipo sawa sawa na programu za mazoezi zinaendelea vizuri, kwa kufanya mazoezi asubuhi na jioni ili kuwaweka tayari na mechi hizo zinazowakabili.

Kiongozi huyo alisema wamekosa mchezo wa kirafiki kama walivyotarajia baada ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kushindwa kuipatia kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza.

"TFF wamejaribu sana kadri ya uwezo wao kuona hilo linafanikiwa kutokana na ratiba kubana imeshindikana kupata mechi ya kirafiki, lakini wanahakikisha kwamba kila kitu kinakuwa sawa ili vijana wapambane kadri ya uwezo wao," Msangi alisema.

Ili kujiandaa na mechi hizo, Poulsen ameita wachezaji 28 ili kupambana kuhakikisha wanapata tiketi ya kushiriki fainali hizo zitakazochezwa Qatar.



Golikipa wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Aishi Manula (katikati), akiwa katika mazoezi ya timu hiyo inayojiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), itakayochezwa Septemba 2, mwaka huu jijini Lubumbashi. **PICHA: TFF**

# *Simba Queens yaiota fainali CAF*

**Na Veronica Ngongona, SAUT**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Hababuu Ali, amesema timu yake inakwenda Nairobi, Kenya kupambana ili kuhakikisha inakata tiketi ya kushiriki Fainali za Klabu za Afrika zitakazofanyika baadaye mwaka huu nchini Misri.

Kikosi hicho kilitarajiwa kuwasili Nairobi jana usiku tayari kwa ajili ya kushiriki michuano hiyo itakayoshirikisha klabu tisa kutoka nchi wanachama wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Akizungumza na gazeti hili, Hababuu alisema kikosi chake kiko tayari kuiwakilisha nchi vyema na hatimaye kuweka rekodi katika mashindano hayo yanayofanyika kwa mara ya kwanza.


Kocha huyo pia aliwaomba Watanzania na mashabiki wote kuisapoti na kuiombea dua timu yao ili kufikia malengo.

"Sisi tunaenda kuiwakilisha nchi, tunaenda kushiriki katika mashindano haya yanayofanyika kwa mara ya kwanza, tunaitaka hii nafasi ili twende kwenye fainali kubwa," alisema Hababuu.

Simba Queens itacheza mechi yake ya kwanza ya hatua ya makundi Jumamosi kucheza dhidi ya PVP FC ya Burundi halafu itashuka tena dimbani Agosti 30 kuvaana na Lady Doves WFC kutoka Uganda na Septemba 3, mwaka huu watamaliza hatua ya makundi kwa kuvaana na FAD FC ya Djibouti.

Timu nyingine zinazoshiriki michuano hiyo zilizoko Kundi B ni pamoja na Yei Joint Stars FC ya Sudan Kusini, New Generation FC ya Zanzibar, Kikosi cha Benki ya Biashara Ethiopia na wenyeji Vihiga Queens.

Michezo
Alhamisi Agosti 26, 2021
Nipashe



Ronaldo alazimisha kurudi EPL
UKURASA 22




Mkurugenzi wa Michezo katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Yusuph Singo (wa pili kushoto), akiwa na viongozi wa klabu ya Yanga katika utambulisho wa jezi zitakazotumiwa na timu yao kwenye mechi za nyumbani na ugenini katika msimu ujao wa 2021/2022. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# YANGA YAFUNGUKA KAZI ZA MANARA

## ●●● Mwenyewe aahidi kufanya mambo mazuri klabuni hapo, kutowaingilia Bumbuli, Nugaz...

**Na Faustine Feliciane**

SIKU moja baada ya aliyekuwa Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, kutangaza kujiunga na klabu hiyo, mabosi wa Yanga wameweka wazi majukumu ambayo yatafanywa na kiongozi huyo, imefahamika.

Manara alitambulishwa rasmi kuhamia Yanga juzi, lakini haikuelezwa atakuwa katika nafasi gani ndani ya klabu hiyo ambayo msimu ujao itashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana jijini Dar es Salaam, Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa, alisema wanachama na mashabiki wamekuwa na wasiwasi juu ya kazi atakazofanya Manara kutokana na uwepo wa Ofisa Mhamasishaji, Antonio Nugaz na Ofisa Habari, Hassan Bumbuli.

Mfikirwa alisema Manara atashughulika zaidi katika idara ya kuhamasisha mashabiki na hiyo itasaidia kuimarisha klabu yao kuelekea kwenye mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji.

"Wakati tunamtangaza Haji (Manara) pale Serena jana (juzi) hatukusema anakuja kufanya kazi gani hasa, lakini niseme uongozi upo makini na haujakurupuka kumchukua Haji, kuna majukumu yapo na ataenda kuyafanyia kazi hasa kutokana na mabadiliko ya klabu yanayofanywa sasa, kutoka katika mfumo wa sasa na kwenda mfumo mpya na wa kisasa zaidi, hatoingiliana na Nugaz na Bumbuli" alisema Mfikirwa na kuendelea.

"Katika mabadiliko ambayo tunayafanya kwa sasa kuna suala la 'fan base', hapa tunahitaji mtu wa kushawishi mashabiki waingie kwenye mfumo rasmi wa klabu baada ya kukamilika taratibu zote, kuna mashabiki mikoa mbalimbali ambao klabu inawahitaji, lakini lazima washawishike, hapa ndipo panapohitajika watu au mtu mwenye kujua kushawishi, kuna nani zaidi ya Manara?, ili ni eneo ambalo tunaamini atafanya kazi kubwa sana kwa manufaa ya klabu," alisema Mfikirwa.

Alisema kila mmoja (Nugaz, Bumbuli na Manara), atafanya kazi yake kwa maendeleo ya klabu na hakutakuwa na mwingiliano.

"Mashabiki wauamini uongozi wao, sisi tupo pale (madarakani) kwa niaba yao, hivyo chochote tutakachokifanya ni kwa faida ya timu hivyo hakuna haja ya kuwa na shaka na ujio wa Manara ndani ya Yanga," Mfikirwa alisema.

Naye Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Wadhamini wa klabu hiyo kutoka GSM, Hersi Said, alisema Manara amekuja kuongeza 'kitu' ndani ya klabu hiyo.

Hersi alisema wanaamini Manara atailetea mafanikio chanya Yanga na uamuzi wa kumchukua umefanywa na umezingatia maslahi ya klabu yao.

Mapema wakati wa uzinduzi wa jezi mpya, Manara alianza kwa kuwapiga kijembe Simba huku akiwaomba mashabiki, wanachama pamoja na viongozi wa klabu hiyo kumpa ushirikiano ili afanye kazi yake kwa ufasaha na weledi.

"Niliyoyafanya kule (Simba), nilipotoka huku nitayafanya mara elfu moja...., nimekuja kwenye klabu kubwa zaidi Afrika Mashariki na Kati, tazama na leo (jana), tunazindua jezi bora zaidi ambayo haina makorokocho, haina pikipiki, haina nazi wala uchafu wowote, hizi ni jezi bora kwa ajili ya timu bora," alisema Manara huku akishangiliwa na baadhi ya mashabiki na viongozi wa klabu hiyo walioudhuria hafla hiyo.

Manara alisema kwa sasa amekuwa na furaha baada ya kupitia 'mambo magumu' na ameishukuru Yanga kwa kumwamini na kumchukua.

Viongozi mbalimbali walihudhuria uzinduzi wa jezi hizo zitakazotumika katika msimu wa 2021/2022 akiwamo Mkurugenzi wa Michezo, Yusuph Singo ambaye alimwakilisha Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, Mkuu wa Wilaya ya Temeke na shabiki wa Yanga, Jokate Mwegelo na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Athuman Nyamlani.

Jezi hizo zilizozinduliwa zitatumika katika mechi za nyumbani na ugenini katika Ligi Kuu Tanzania Bara, michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, pamoja na jezi kwa ajili safari kwa wachezaji, benchi la ufundi na viongozi.

## Simba dimbani tena Morocco

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Simba ambacho bado kinaendelea na mazoezi yake Morocco kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya, kinatarajia kushuka dimbani kucheza mechi nyingine ya kirafiki ya kimataifa dhidi Olympique Club de Khouribga itakayochezwa leo nchini humo.

Kaimu Ofisa Habari wa Simba, Ezikiel Kamwaga, aliliambia gazeti hili Kocha Mkuu, Didier Gomes amehitaji kikosi chake kicheze mchezo mwingine wa kirafiki ili kuwajenga ikiwa ni sehemu ya programu za mazoezi alizoziandaa kwa timu yake.

Kamwaga alisema Gomes anaamini mechi hiyo itaendelea kuwaweka wachezaji wao 'fiti' na kuimarisha uelewano wa wachezaji ambao baadhi yao ni wapya kwenye kikosi hicho.

"Programu iliyopo kwa sasa ni timu kuendelea kubaki nchini Morocco na kesho (leo), tutacheza mechi ya pili ya kirafiki na Olympique Club de Khouribga, ambayo itakuwa pia ya kuwaangalia kiufundi zaidi wachezaji, hizi mechi zinamsaidia kuona wachezaji wapya na wazamani walipofikia, " alisema Kamwaga.

Kocha huyo amewataka mashabiki kuendelea kuwa watulivu, kuhusu maendeleo ya timu hiyo ambayo iko sehemu tulivu na itakaporejea watakuwa na kazi moja ya kuhakikisha wanapambana ili kupata matokeo mazuri.

"Nafurahishwa na namna ambavyo wachezaji wangu wanafanya, ni furaha kwangu na kwao pia, kikubwa sio matokeo bali ni jinsi gani walivyofanya na kile ambacho niliwapa katika mazoezi, bado tuna mwezi mmoja wa kufanya kazi na maandalizi zaidi, tuna muda wa kujiaandaa kwa ajili ya msimu ujao na ninafurahishwa na kile ambacho wachezaji wanakifanya,"alisema Gomes.

Simba ikiwa nchini humo tayari wamecheza mchezo mmoja wa kirafiki dhidi ya FAR Rabat ulimalizika kwa sare ya mabao 2-2.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >